# Nipashe

Jumamosi Mei 30, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580245

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Mume na mke wadaiwa kujinyonga wivu mapenzi

UKURASA 18




UKURASA 11

# Zitto afungwa mwaka mmoja

UKURASA 2



Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe (kulia), akitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuhukumiwa kutumikia kifungo cha nje cha mwaka mmoja, baada ya kukutwa na hatia ya makosa matatu ya uchochezi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## BAA LA CORONA



Hakikisha unatupa vifaa vyote ambavyo vinatakiwa kutupwa baada ya kutumika kama glovu na barakoa wakati unapofanya usafi. Usifue na kuvaa tena. WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## NAIBU SPIKA ASAKA JIMBO

UKURASA 4

# Bodi ya Mikopo yatoa bil.123/- kwa wanavyuo

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** SIMBA, AZAM PATACHIMBIKA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Bodi ya Mikopo yatoa bil. 123/-

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imetoa Sh. bilioni 122.8 kwa vyuo na taasisi mbalimbali za elimu nchini kwa ajili ya ada, chakula na malazi ya wanafunzi wanaorejea vyuoni kuendelea na masomo Jumatatu.

Mkurugenzi wa HESLB, Abdul Razaq Badru, aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari.

Alibainisha kuwa, kati ya kiasi hicho, Sh. bilioni 63.7 ni kwa ajili ya chakula na malazi kwa wanafunzi 132,119 kupitia vyuo na taasisi za elimu 81 kwa kipindi cha miezi miwili kwanzia Juni Mosi hadi Julai 30, mwaka huu na kiasi kingine cha fedha ni malipo ya ada.

Alisema malipo ya robo ya nne ambayo ni ya mwisho kwa mwaka huu wa masomo, yatalipwa mwishoni mwa Julai mwaka huu.

Badru alisema kuwa katika kipindi cha wiki moja iliyopita kuanzia Mei 21 hadi Mei 29, mwaka huu, Sh. bilioni 59.1 zilipelekwa vyuoni kwa ajili ya ada za wanafunzi wanufaika ambazo zimelipwa kwa taasisi za elimu ya juu zaidi ya 70 nchini. "Ni matumaini yetu kuwa fedha hizi zitavisaidia vyuo kutoa huduma bora kwa wateja wetu wapatao 132,119 waliopo katika taasisi za elimu mbalimbali nchini kote," alisema.

Vilevile, alisema tayari bodi imeshapeleka maofisa mikopo vyuoni kwa ajili ya kushughulikia mikopo ya wanafunzi.

Alisema wanafunzi wasiogope kurudi vyuoni kuendelea na masomo kwa sababu serikali imejipanga kwa kila kitu na kuwataka kuanza kuripoti kwa ajili ya kujisajili.

"Ninaomba wanafunzi wasiogope warudi shuleni, ili kuendelea na masomo kama ambavyo imetangazwa na serikali kuanzia Juni Mosi, mwaka huu," alisema.

Alisema usajili wa wanafunzi ulianza juzi na utaendelea hadi kesho, lakini watakaochelewa usajili utaendelea kufanyika Jumatatu.

Badru alisema Benki za biashara ziko tayari kwa ajili ya kusaidia mchakato wa malipo ya mikopo kwa wanafunzi wa vyuo.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), Faustine Bee, alisema chuo chake kimezingatia suala la corona, akibainisha kuwa wanafunzi watakuwa na barakoa na vitakasa mikono kwa ili kuendelea kujikinga na ugonjwa huo. Profesa Bee alisema chuo kina vitakasa mikono na maji tiririka ambayo watayatumia kwa ajili ya kujilinda dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona.

"Wanafunzi wote wanatakiwa waripoti kama maelezo yalivyotolewa na serikali ili kuwahi kuanza masomo kwa mujibu wa ratiba," alisema. Machi 17, mwaka huu, serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ilitangaza kufunga shule na vyuo vyote ikiwa ni siku moja baada ya Tanzania kuripoti kisa cha kwanza cha corona.



Rais John Magufuli akichota mchanga kuweka kwenye toroli wakati alipoenda kuangalia maendeleo ya ujenzi wa ofisi za Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana **PICHA: IKULU**

# Zitto ahukumiwa kifungo cha nje mwaka 1

**Na Hellen Mwango**

MBUNGE wa Kigoma Mjini wa Chama cha ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe, amehukumiwa kutumikia kifungo cha nje cha mwaka mmoja baada ya kukutwa na hatia ya makosa matatu ya uchochezi.

Kadhalika, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu imemwamuru kutoandika na kutoa maneno ya uchochezi kwa muda wa mwaka mmoja.

Hukumu hiyo imetolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi 15 wa Jamhuri na wanane wa utetezi akiwamo Zitto mwenyewe.

Alisema, maneno aliyoyatoa Zitto hayana ukweli, makali na magumu mno ambayo yameshindwa kuthibitishwa kwenye utetezi wake mahakamani.

"Mahakama hii bila kuacha shaka imeona utetezi wa mshtakiwa umeshindwa kuthibitisha kwamba askari wamemuua nani na ushahidi unaonyesha tukio lilifanyika alfajiri muda ambao huwezi kusema nani alimuua nani, maneno yalikuwa mazito, watu 100 kufa sio kitu kidogo mpaka kutaja watu wa kabila fulani hii ni sawa na kuwasha moto kwenye nyasi kavu," alisema.

Alisema jamii ina watu wenye uelewa tofauti kutokana na uwezo wa kuchuja maneno, hivyo kila mmoja anaweza kuchuja kwa kadiri anavyoweza.

"Mahakama hii imekuona una hatia, inakutia hatiani kwa makosa yote matatu, mmezoea kuandika mitandaoni kwamba Kisutu imegeuka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), mshitakiwa utatumikia kifungo cha nje cha mwaka mmoja kwa masharti, usiandike na kutoa maneno ya uchochezi kwa muda huo," alisema Hakimu Shaidi.

Alisema kama kuna upande ambao haujaridhika na hukumu hiyo una haki ya kukata rufani ndani ya siku 30.

Awali, Upande wa Jamhuri uliopokea hukumu hiyo uliongozwa na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Renatus Mkude na Wankyo Simon.

Mkude alidai kuwa Jamhuri inaomba mahakama kutoa adhabu kali kwa Zitto ili iwe fundisho kwake na kwa wengine.

Hata hivyo, wakili wa utetezi, Frank Mwakibolwa, aliiomba mahakama kuwa mshtakiwa ana familia inayomtegemea, baba wa watoto wadogo wanne na ni mkosaji wa mara ya kwanza.

Wakati wa usikilizwaji wa ushahidi, kesi hiyo iliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, huku upande wa utetezi ukiongozwa na mawakili Jebra Kambole, Mwakibolwa na Bonifacia Mapunda.

Kadhalika, wakati wa kipindi cha usikilizwaji wa kesi hiyo upande wa mashtaka uliwasilisha mahakamani vielelezo vya nyaraka na video iliyodaiwa kurekodiwa na askari mpelelezi, Sajenti James, kwenye mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika jijini Dar es Salaam, Oktoba 28, 2018.

Video hiyo iliwasilishwa mahakamani hapo Desemba 4, 2019, na kupokelewa baada ya mabishano huku upande wa utetezi ukitaka video hiyo isipokelewe, lakini hatimaye mahakama ilipokea ushahidi huo na video hiyo ilionyeshwa.

Katika kesi ya msingi ilidaiwa kuwa Oktoba 28, 2018, Zitto aliitisha mkutano wa waandishi wa habari uliofanyika ofisi za Makao Makuu ya ACT-Wazalendo, uliodaiwa kuwa na lengo la kuleta chuki kwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinyume na sheria na kwamba alitoa maneno ya uchochezi dhidi ya Jeshi la Polisi.

# Askofu atoa hadhari corona

**Na Mary Geofrey**

ASKOFU wa Kanisa la Waadvetista Wasabato Jimbo la Kusini, Mark Malekana, amewataka Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya virusi ya corona licha ya Tanzania kufanikiwa kupunguza maambukizo.

Amesema Rais John Magufuli amesaidia kuondoa na kumaliza hofu iliyokuwa imetanda nchini ambayo ilikuwa ikiondoa maisha ya Watanzania na kufanya maambukizo kupungua.

Askofu Malekana alitoa wito huo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari katika hafla ya kukabidhi vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona zikiwamo barakoa, vitakasa mikono na vifaa vya kujikinga vya wataalamu wa afya vyenye thamani ya Sh. milioni nane kwa Manispaa ya Temeke.

Alisema misaada hiyo ni mwendelezo wa misaada yenye thamani ya Sh. milioni 100 iliyotolewa na Shirika la Maendeleo na Misaada Wakati wa Maafa la Kisabato (Adra Tanzania) kwa udhamini wa Taasisi ya LDS.

Alisema jitihada hizo zinakwenda sambamba na kuchapisha vipeperushi vya kutoa elimu kwa jamii kujikinga na maambukizo hayo.

"Ujasiri usiwaondolee tahadhari, tumetiwa moyo ili tusife kwa hofu ya corona. Tuendelee kuzingatia tahadhari zinazotolewa na Wizara ya Afya na tuache kupokea taarifa kutoka vijiweni, masokoni na watu wasiohusika katika hili," Askofu Malekana alionya.

Kiongozi huyo wa kiroho pia aliwataka Watanzania kuendelea na utaratibu wa kunawa mikono mara kwa mara kwa sababu unaepusha maradhi mbalimbali ya kuambukiza.

Vilevile, alivitaka vyuo vyote na wamiliki wa shule za sekondari na msingi nchini, kutoingilia ratiba za kumwabudu Mungu katika siku zilizopangwa kwa waumini wa dini zote kwa kisingizio cha ratiba za masomo kubana.

"Vyuo na shule zinaanza kufunguliwa tunawaomba wahusika wote kuzingatia ratiba za kumuabudu Mungu na siyo walimu wanaanza kupanga ratiba za masomo na mitihani na kutoweka siku za kuabudu kwa kisingizio muda hautoshi, tuheshimu ratiba za kumwabudu Mungu maana bila yeye tusingeishinda hofu iliyokuwa mbele yetu," alisema.

Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Manispaa ya Temeke, Grace Ntangu, aliwashukuru kwa msaada waliowapatia na kuahidi kuwafikia walengwa wote.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), mkoa wa Tanga, Dk. Sharifa Bungala, akizungumza na waandishi wa habari jijini Tanga jana, kuhusu kuokolewa kwa fedha za wazazi na walezi wa wanafunzi wa kidato cha sita wanaosoma shule ya St. Marys, iliyopo wilayani Lushoto, kiasi cha Sh. 133, kwaajili ya malipo ya ziada kabla kufunguliwa kwa shule. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Takukuru yaokoa mil. 134/- ada Mazinde Juu

**Na Boniface Gideon, TANGA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) imeokoa Sh. 134,500,000 zilizotarajiwa kukusanywa na Shule ya St Mary's Mazinde Juu, wilayani Lushoto kutoka kwa wazazi na walezi kwaajili ya malipo ya ziada ya ada kabla ya Juni mosi, siku ambayo wanafunzi wa kidato cha sita wanatarajia kuanza rasmi masomo baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Akizungumza jana, Mkuu wa Takukuru, Mkoa wa Tanga, Dk. Sharifa Bungala, alisema taasisi hiyo ilipokea malalamiko kutoka kwa wazazi na walezi wa wanafunzi wanaosoma shuleni hapo kidato cha sita, kwamba wamepewa maagizo kupitia kundi la 'WhatsApp' la wazazi na walezi kuanza kulipa fedha za ziada kabla ya kuanza kuwarudisha watoto wao shuleni kuanza masomo.

Bungala alisema malalamiko hayo yalikuwa yakimtuhumu Mwalimu Mkuu wa shule hiyo. "Wazazi na walezi walilalamikia mkuu wa shule hiyo kuwa amewaagiza waanze kulipa kiasi cha Sh. 750,000 kwa kila mwanafunzi kabla ya Juni mosi, inadaiwa kuwa fedha hizo zilikuwa ni kwaajili ya kuwalipa walimu na wafanyakazi ambao watakuwapo katika kipindi hiki wanafunzi wakiwa shuleni kujiandaa na mitihani ya kuhitimu kidato cha sita."

Alisema suala hilo la malipo ya ziada lilionekana kuwakera wazazi na walezi wenye wanafunzi. "Wazazi wengi hawakufurahishwa na kitendo hicho kwasababu wengi wao wanaeleza kuwa walikuwa wameshalipa ada inayotakiwa kabla ya kufungwa kwa shule baada ya kuibuka kwa janga la corona na kimsingi hawakutakiwa kudai malipo ya ziada."

Malalamiko mengine ya wazazi na walezi ni kuhusu malipo ambayo walishayalipa Sh. 100,000 kwa kila mwanafunzi ili wabakie shuleni hapo kwa ajili ya kujiandaa na mitihani wakati wa likizo.

Kufuatia malalamiko hayo, Takukuru ilifanya ufuatiliaji kwa kuwasiliana na uongozi wa shule hiyo na kuthibitisha kuwa tuhuma hizo ni za kweli na kwamba wazazi na walezi wa wanafunzi 178 kati ya 222 wa kidato cha sita walitakiwa kulipa kiasi hicho fedha Sh. 750,000 kabla ya kufunguliwa kwa shule.

"Wanafunzi 44 wanaosoma shuleni hapo malipo hayo hayakuwahusu kwa kuwa wana ufadhili wa shule na wafadhili mbalimbali," alisema Bungala.

Alisema Sh. 133,500,000 zilitarajiwa kukusanywa na shule hiyo kutokana na malipo hayo na tayari wazazi wa wanafunzi wanne walikuwa wameshalipa jumla ya Sh. 3,000,000. "Tulipouhoji kwa lengo la kupata ufafanuzi wa tuhuma hizo, Mkuu wa shule hiyo alisema wazo la malipo hayo lilifanywa na wazazi na walezi wenyewe kupitia kundi lao la WhatsApp na kwamba alikubaliana nao baada ya kuona kuwa ni jambo jema, lakini alipoona mjadala huo umekuwa mkali aliwaeleza kuwa malipo hayo siyo ya lazima bali atakayependa alipe na ambaye hawezi asilipe."

Alisema baada ya kuchambua maelezo ya Mkuu wa shule hiyo na ushahidi uliopatikana Takukuru na uongozi wa shule, walikubaliana baadhi ya mambo ili kuondoa malalamiko hayo ikiwamo kuandikwa kwa waraka wa kufuta mjadala huo wa malipo ya ziada ikieleza hakuna malipo hayo pamoja na kurejeshwa kwa fedha kwa wazazi na walezi ambao walikuwa wameshalipa.

# Wema wamponza, wageni aliowapa hifadhi wamuua

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linawasaka watu wasiofahamika kwa tuhuma za kumuua kwa kumkata mapanga Mandago Mboje (30), mkazi wa kijiji cha Kizi, kata ya Paramawe, tarafa ya Namanyere, wilayani Nkasi.

Akitoa taarifa za tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justine Masejo, alisema lilitokea usiku wa Mei 26, majira ya saa 2.00 usiku baada ya watuhumiwa hao kufika nyumbani kwa marehemu na kuomba hifadhi.

Kamanda Masejo alisema, kabla ya kuuawa, watu hao walifika kwenye nyumba ya marehemu na kuomba hifadhi wakidai kuwa ni wageni katika kijiji hicho wakitafuta ng'ombe wao waliopotea.

Alisema waliomba walale nyumbani hapo ili kesho yake waendelee na kazi ya kuwatafuta ng'ombe hao katika mazizi yaliyopo kijijini hapo.

Kamanda alisema, baada ya kupokelewa kwa ukarimu, walipewa chakula cha jioni na kuandaliwa maji ya kuoga na kisha kuonyeshwa sehemu ya kulala.

Alisema walipoingia chumbani kulala, baada ya muda mfupi wageni hao waliamka na kwenda kwenye chumba alichokuwa amelala mwenyeji wao na kisha kumvamia na kumkata mapanga sehemu mbalimbali za mwili wake.

Kamanda alisema walipohakikisha kuwa amekufa, walitoka ndani ya nyumba hiyo na kutimua mbio kukimbilia kusikojulikana na hawajakamatwa mpaka sasa kwa kuwa majirani hawakuwa na taarifa ya ugeni huo na pia serikali ya kijiji haikuwa na taarifa ya uwapo wa wageni hao kijijini.

Polisi inaendelea na uchunguzi kuwabaini watu waliofanya mauaji hayo ili wafikishwe mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Kamanda aliwaonya wakazi wa mkoa huo kuacha kuwapokea wageni wasio wafahamu na kuwapa hifadhi bila kushirikisha viongozi wa serikali wa eneo husika kwa kuwa ni hatari kwao na familia zao kutokana na wengine kuwa majambazi.

**Kamanda Masejo alisema, kabla ya kuuawa, watu hao walifika kwenye nyumba ya marehemu na kuomba hifadhi wakidai kuwa ni wageni katika kijiji hicho wakitafuta ng'ombe wao waliopotea.**


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**OFISI ZA TRA KUWA WAZI JUMAMOSI NA JUMAPILI NCHI NZIMA**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuutaarifu Umma kuwa, ofisi za TRA nchi nzima zitakua wazi siku ya **Jumamosi** tarehe **30 Mei, 2020** na **Jumapili** tarehe **31 Mei, 2020** kwa ajili ya kutoa huduma kwa walipakodi kuanzia **saa 2:30 asubuhi** hadi **saa 11:00 jioni.**

**WOTE MNAKARIBISHWA!**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi**
**TRA MAKAO MAKUU**

# Naibu Spika: Nitawania ubunge, jimbo nitalitaja

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

NAIBU Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema ana nia ya kugombea ubunge katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu kwenye jimbo ambalo atalitaja wakati ukifika.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini hapa katika kikao cha kuwapongeza wabunge na mawaziri wanawake kwa utendaji kazi wao kwa kipindi cha miaka mitano kilichoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema anayo nia ya kugombea ubunge na viongozi wao wamesisitiza suala la kufuata utaratibu, hivyo muda utakapofika, atabainisha jimbo analolinyatia.

"Nia ninayo ya kugombea, nitagombea wapi, tutaelewana baadaye kidogo, ninatamani nia hiyo itimie nishinde, ili kura zitakazopatikana zikiwa nyingi zilete wabunge wa viti maalum,"alisema.

Naibu Spika huyo alisema wanawake wanaojitokeza kugombea, watiwe moyo kwa kuwa wanatamani wawe wengi kwenye majimbo na kuongeza idadi yao ya viti maalum.

"Tunamshukuru Rais kwa kuwaamini wanawake na tunaamini hawajamwangusha, wale wenzangu tunaokwenda kutia nia, tumetiwa moyo na viongozi wetu wa UWT kuwa watakuwa nasi katika hiyo safari, wapo viti maalum wanataka kugombea majimbo na wengine hawajaamuaamua hivi, lakini kwa kauli ya leo (jana) ya Mwenyekiti tumetiwa moyo," alisema.

Aliomba uongozi wa UWT kushugulikia mvutano wa wabunge wanawake ambao alibainisha kuwa wanasuguana na wabunge wanaume kuwania majimbo na kwamba, yeye kama msaidizi wa Spika, ameyasikia hayo mengi.

"Wapo wabunge wa viti maalum wanavutana, utafikiri ndani walikuja kwa kuvutana, lakini kila mtu anatakiwa kufanya kazi yake, sisi wote ni wanaCCM, hakuna haja ya kuvutana, tunapoteza nguvu nyingi sana kwenye kuvutana badala ya kufanya kazi ya kuonyesha wanawake tunaweza," alisema.

Awali, akifungua kikao hicho, Mwenyekiti wa UWT Taifa, Gaudencia Kabaka, aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea kwenye majimbo na kutosubiri nafasi za viti maalum.

"Mara nyingi tunafikiri kwamba ubunge wa jimbo ndiyo imara zaidi, tumeanza kuhangaishana wanawake kwa wanawake kwenye majimbo hilo suala nimelipata, tukubaliane nani wa kwenda jimboni na nani viti maalum," alisema.

Alisisitiza kuwa ili kuongeza idadi ya wanawake bungeni, lazima waende kugombea majimbo kwa kuwa mchakato wa kuchagua wabunge wa viti maalum unategemea kura za Rais na wabunge wa majimbo.

Aliomba katika vikao vya kuchuja na kutoa majina matatu ya wagombea kuhakikisha jina la mwanamke halikosekani.

"Wanawake wenye majimbo msiyaache, tutahangaika na chama hata ukiwa namba mbili au tatu, mchakato wa kwanza ni lazima mteuliwe, hivyo lazima jina la mwanamke liwapo, ninawahakikishia tutagangamala na chama," alisema.

Vilevile, alimwomba Rais kuendelea kuteua wanawake katika baraza lake la mawaziri, ili kufika walau asilimia 30.

Mwenyekiti wa wabunge wanawake wenye majimbo ambaye ni Mbunge wa Ileje, Janeth Mbene, alisema kuna vita kubwa kwenye majimbo na kushukuru kauli ya kiongozi wa umoja huo kwa kuwahakikishia kulinda nafasi zao.

"Tunajua utaratibu lazima ufuatwe, ndiyo demokrasia, tutachukua fomu, pale ambapo kuna mwanamke na sifa, jina lake lirudi, lisikatwe. Bado kuna mizengwe na mambo mengi yanaweza kutokea," alisema.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, ambaye pia ni Mbunge wa Ilemela, alikiomba chama kuwaonya viongozi wa ngazi za chini ambao kwa sasa wanawatambulisha wagombea wakati muda bado haujafika.

"Kuna kitu kinaendelea siyo kwa majimbo yote na kwa sehemu kubwa kinalelewa na viongozi hasa wa chama. Kwa mfano, unaingia kwenye kikao cha kamati ya siasa, kiongozi anasema kiongozi yeyote anaruhusiwa kumpokea mgombea na kumtambulisha wakati Bunge bado linaendelea na madiwani bado," alisema.

Naye Mbunge wa Welezo, Saada Mkuya, alisema mwaka huu, Zanzibar kutakuwa na uchaguzi wa Rais, hivyo akaiomba UWT kuweka msukumo wa wanawake kugombea nafasi za juu katika uchaguzi huo.

## Hapi atoa wiki mbili bil. 9/- kulipwa

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) na Kamanda wa Polisi mkoa huo, kufika ofisini kwake pamoja na wakurugenzi watendaji wa kampuni za chai, kujieleza sababu za kupuuza agizo la serikali la kulipa mapato ya Sh. bilioni tisa kati ya bilioni 11.7 walizokuwa wakidaiwa.

Akitoa agizo hilo jana, katika kikao cha Baraza Maalum la Madiwani la Halmashauri ya Mufindi, Hapi alisema, awali uliibuka mgogoro wa wenye viwanda hao kuhusu kodi na kusababisha ofisi yake kuunda tume maalumu ya ufuatiliaji na uamuzi ulikuja kutaka kampuni hizo kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa madai hayo, walikuwa wakidaiwa Sh. bilioni 11.7 na walikuwa wamelipa Sh. bilioni mbili.

Alisema tangu walipopewa agizo hilo Machi 12, mwaka huu, hadi sasa hazijatekeleza, hivyo anaona ni upuuzaji mkubwa na kwa kuwa nchi inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ni lazima kila mmoja atii sheria iliyowekwa.

"Nimeona katika hili mnataka kuleta dharau sasa katika hili, ninawapa wiki mbili wakurugenzi wote wa kampuni ya chai Mufindi kwa maana na Kisigo, Uniliver na MCT kufika ofisini kwangu kujieleza kwanini wameshindwa kutekeleza agizo la serikali la kulipa mapato ...nasema Juni 2, wakurugenzi wote mfike ofisini pia Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Mkurugenzi Takukuru na Jeshi la Polisi," alisema.Alisema, nchi haiwezi kuongozwa kama watu wachache wanafanya mchezo wa kulipa kodi ya serikali kwa kuona wapo juu ya sheria.

Pia, alisema serikali inahitaji viwanda vifanye kazi, lakini lazima viwanda hivyo viweze kulipa kodi ya serikali kwa wakati na kwa mujibu wa sheria na kuwa katika suala hilo la mapato hakuna mtu anayeweza kuwaokoa wenye viwanda hao kuendelea kuendesha viwanda vyao pasipo kulipa kodi.

Katika hatua nyingine, Hapi aliitaka halmashauri hiyo kuhakikisha inaweka utaratibu wa kukusanya madeni ya Sh. 55,586,413 yanayotokana na wakusanyaji wa mapato katika vyanzo mbalimbali kama ilivyobainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2018/2019.



Mtafiti wa dawa ya asili, Rose Roberty (Changa Muja), akiwaonyesha waandishi wa habari dawa aliyogundua ya kutibu ugonjwa wa Corona nyumbani kwake katika Mtaa wa Masailand, Kata ya Olorieni, wilayani Arumeru, mkoani Arusha juzi, ambapo ameiomba serikali imsaidie kuichukua ili kuipima na kuifanyia majaribio. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Waziri akoshwa utoaji elimu ya corona TPSC

**Na Mwandishi Wetu, SINGIDA**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, amepongeza mpango uliowekwa na Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) wa kila mwalimu kabla ya masomo, kuelimisha kuhusu corona.

Chuo hicho kimeunda vikosi kazi katika kampasi zake vitakavyokuwa na jukumu la kusimamia shughuli za uelimishaji wanachuo dhidi ya corona.

Dk. Mwanjelwa alitoa pongezi hizo jana wakati akiwa katika ziara ya kikazi kwenye chuo hicho, Kampasi ya Singida.

Katika ziara hiyo, Mtendaji Mkuu na Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Emmanuel Shindika, alieleza mikakati wa uendeshaji mafunzo kwa kuzingatia tahadhari dhidi ya corona itakayoanza kutekelezwa kuanzia Jumatatu.

Akiwa ziarani humo, Dk. Mwanjelwa alikipongeza chuo hicho kwa kushughulikia dharura zitakazojitokeza kutokana na ugonjwa huo ikiwa ni sehemu ya mkakati mahususi katika kutekeleza agizo la Rais John Magufuli.

"Nimeridhishwa na jitihada za chuo za kuweka mabomba ya maji tiririka nje ya geti ili kuwawezesha wafanyakazi, wanafunzi na wadau wa chuo kunawa mikono yao na sabuni kwa maji tiririka ambapo walinzi getini watakuwa wakisimamia," alisifu.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Shindika, alisema vikosi kazi hivyo vilivyoundwa, pia vitakuwa na jukumu la kukagua miundombinu na kutendea kazi ili kujiridhisha na ubora wake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kunakuwa na maji tiririka ya bomba na sabuni.

"Tunashukuru kwa kututembelea ili kujiridhisha na mkakati wa chuo katika kukabiliana na corona kabla ya vyuo kufunguliwa, tumefanya tathmini na kuainisha maeneo hatarishi kwa maambukizo na hatimaye kuandaa mkakati madhubuti wa uendeshaji wa mafunzo kwa kuzingatia tahadhari dhidi ya maambukizo ya corona;" alisema.

Mei 21, mwaka huu, Rais Magufuli alitangaza kufunguliwa kwa vyuo vyote nchini ifikapo Jumatatu baada ya serikali kutangaza kuvifunga Machi 17 , mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# 'Utalii umerejea, tahadhari corona lazima ichukuliwe'

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, amesema utalii nchini lazima uendelee licha ya kuwapo kwa janga la corona ambalo ni tishio duniani.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa video maalum za kutambulisha utalii wa Tanzania, Dk. Kigwangalla alisema janga la corona limeathiri kwa kiwango kikubwa sekta ya utalii nchini na hivyo kuathiri uchumi wa nchi pia.

Hata hivyo, waziri huyo alisema kwa sasa dalili za kurejea kwa utalii katika hali yake ya kawaida zimeanza kuonekana baada ya watalii kuanza kuingia nchini.

"Sasa hivi soko la utalii duniani limeathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na ugonjwa wa corona, lakini nchi mbalimbali zimeamua kuanza kufungua biashara ya utalii na biashara ya usafiri wa anga na usafiri wa majini na zingine zinazoendana na sekta ya utalii.

"Kwa msingi huo, kama tungeendelea kuweka masharti yaliyokuwapo, sekta hii isingeweza kufunguka kama vile katika mataifa mengine walioanza kufungua utalii kwenye nchi zao," alisema.

Akizindua video hizo maalum zilizopewa jina 'Tanzania Unforgettable' (Tanzania Haisahauliki) zikitengenezwa kwa lugha mbalimbali zikiwamo Kiingereza, Kiswahili, Kichina, Kiisraeli na Kifaransa, waziri huyo alisema lengo lake ni kuitangaza Tanzania kiutalii katika mataifa mbalimbali duniani.

"Video hizi kuna ya dakika tatu, dakika saba na dakika 10. Ninatoa rai kwa Watanzania wote, wadau mbalimbali wa utalii, washiriki kuisambaza video hii ili kuwavuta wote na kukonga nyoyo za watakaoitazama video hiyo ambayo inaelezea vivutio mbalimbali vilivyopo Tanzania," aliomba.

Alisema wizara hiyo imeweka mwongozo ambao unaelekeza hatua muhimu za kufanya, ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona na kuwataka watalii na wananchi wanaohudumia watalii hao, kufuata mwongozo huo kujilinda dhidi ya hatari ya maambukizo ya corona.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (aliyevaa barakoa), akikagua ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Kwimba, inayojengwa katika eneo la Icheja jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Vijana 500 Chadema kuwania udiwani, ubunge

**Na Enock Charles**

BARAZA la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), limesema wapo vijana zaidi ya 500 walioijitokeza kuwania nafasi za udiwani na ubunge kutoka katika chama hicho katika kata na majimbo mbalimbali nchini.

Akizungumza katika gumzo la Nipashe linalofanyika katika ukurasa wa mtandao wa kijamii wa twita, Mwenyekiti wa Baraza hilo, John Pambalu, alisema kujitokeza kwa vijana hao ni ishara ya hamasa iliyopo katika taifa kwa sasa katika kupigania maendeleo ya nchi yao.

"Vijana katika taifa lolote ndio wachochezi wakubwa wa maendeleo ya nchi, sisi kama vijana tunapata faraja kuona idadi hiyo kubwa ikijitokeza kuwania nafasi hizo ni ishara ya mafanikio kwetu," alisema Pambalu

Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani, unatarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu huku kila chama kikipanga mikakati yake na kuandaa wagombea katika uchaguzi huo, wakati chama hicho kikuu cha upinzani nchini kikifunga hatua ya watu kujitokeza kutia nia kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, Chama cha ACT- Wazalendo, kilifungua hatua hiyo mwezi uliopita.

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT -Wazalendo, Ado Shaibu, aliagiza tangu Aprili 30, mwaka huu, makatibu wa kata na majimbo wa chama hicho kuandaa madaftari ya kuorodhesha watia nia katika maeneo yao ili kupata idadi ya watia nia katika chama hicho.

Aliwataka watia nia hao kuzingatia maadili, utu na utamaduni wa chama hicho wanapotangaza nia zao hizo na kuomba msaada wa kuunganishwa na vyombo vya habari ili kujitangaza inapobidi katika idara ya uenezi ya chama hicho, mpaka sasa wanachama kadhaa wa chama hicho wakiwamo vijana wamekwisha jitokeza hadharani kutangaza nia.

# Wanafunzi wapata ajali wakirejea shuleni

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WANAFUNZI kutoka vyuo mbalimbali na wanafunzi wa kidato cha sita wanaosoma jijini Mbeya, wamenusurika kifo baada ya basi ya Premier lenye namba za usajili T, 629 AET, walilokuwa wakisafiria kutoka Mwanza kwenda Mbeya, jana saa 3 asubuhi, kupata ajali katika eneo la Ngaganulwa Usanda, wilayani Shinyanga.

Abiria walionusurika kwenye ajali hiyo akiwamo Justice Alyoce, mwanafunzi wa kidato cha sita, alisema wakati wakiwa njiani wakitokea Mwanza, basi hilo lilikuwa likifukuzana na Abood na walipofika eneo hilo wakapata ajali.

Alisema katika eneo hilo la Ngaganulwa, basi la Abood lililokuwa mbele lilisimama upande wa kushoto na upande wa kulia kulikuwa na basi jingine la Allys, ndipo dereva la basi la Premier alipoanza kufunga breki na kumshinda na kisha kuanguka.

"Wakati tukitokea Mwanza kwenda Mbeya shuleni na wengine vyuoni, tulipokuwa njiani basi letu la Premier pamoja na Abood yalikuwa yakifukuzana huku madereva wakipigiana honi walipokuwa akimpita mwezake, na tulipofika hapa wakati tukiwa mwendokasi ndipo tukakutana na mabasi yamesimama na hatimaye kupata ajali,"alisema Aloyce.

Kwa upande wake Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba ambaye alikuwa eneo la tukio, alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi, dereva wa basi la Premier alipofika eneo hilo na kukuta mabasi mawili yamesimama pande zote basi lilimshinda na hatimaye kuanguka.

Alisema basi hilo lilikuwa limebeba abiria 59, wengi wao wakiwa wanafunzi wa kidato cha sita pamoja na vyuo, huku akiwataja majeruhi saba wa ajali hiyo kuwa ni Thabiti Abdul, Swaum Kisandu, Mohamed Nyerere, Betha Minami, Mohamed Ahmed, Ilham Yahya, pamoja na Haida Hassani.

Alisema Majeruhi hao wote wamepata majeraha katika maeneo mbalimbali ya viungo vya miili yao na kukimbizwa kituo cha afya Tinde, kilichopo karibu na eneo la ajali, huku kukiwa hakuna kifo na kubainisha wanamtafuta dereva wa basi hilo ambaye amekimbia.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wachezaji, viongozi Bara wakumbushwa nidhamu

RAIS Dk. John Pombe Mafuguli ametangaza kuifungulia rasmi michezo yote hapa nchini kuanzia Juni Mosi, mwaka huu.

Kauli hii ni ishara kuwa wanamichezo wote wanatakiwa kujiandaa kumalizia kalenda zao za mashindano ya mwaka huu au msimu kwa upande wa soka.

Michezo ambayo imefunguliwa ni pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na Ligi Kuu Zanzibar ambazo zilikuwa zimesimama kwa ajili ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Kutokana na janga hilo, wachezaji wa ligi hizo wote walikuwa wakifanya mazoezi binafsi ili kulinda viwango vyao kwa kufuata programu maalumu walizopewa na makocha wao.

Wanamichezo hao walitakiwa kujiimarisha ili waendelee kupambana kuwania mataji mbalimbali, pale walipoishia kwa kuamini msimu wa ligi au shindano, humalizika siku ya mwisho.

Pamoja na kauli ya Rais Magufuli kufungua michezo, bado wanamichezo wote wanatakiwa kujifua kwa kufuata tahadhari zilizotolewa na wataalmu wa afya, kwa sababu bado corona haijamalizika.

Wachezaji wanaporejea uwanjani, hasa nyota wetu wanaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, wanatakiwa kuhakikisha wanafuata na kuheshimu kanuni, sheria na taratibu zilizowekwa.

Kwa kufanya hivi, kutawasaidia wachezaji hao kutimiza malengo ya timu zao, kwa sababu bado ni mapema kukata tamaa.

Kwa mfano katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, timu zimebakisha kati ya michezo tisa na 11, hapo klabu itakayopata matokeo chanya inaweza kuwashangaza wengine kwa kumaliza kwenye nafasi ya juu katika msimamo.

Hii pia uko katika upande wa wale ambao walionekana wako kwenye janga la kushuka daraja kwa kuvuna pointi na kujiondoa kwenye hatari hiyo.

Nipashe inawakumbusha wachezaji na viongozi, wakati huu hasa baada ya ligi kurejea, ni wakati muhimu ambao unaonyesha taswira za klabu na wachezaji wetu ambao walitumia vibaya mapumziko ya corona kwa kuharibu viwango vyao.

Mbali na kumaliza msimu, kipindi kilichobakia ni muhimu zaidi kwa wachezaji kwa sababu kinaelekea na usajili, ili mchezaji upate soko la kutakiwa na klabu nyingine au kupanda dau hapo ulipo, ni lazima uwe na nidhamu.

Mchezaji ambaye hana nidhamu, huwa na nafasi ndogo katika mafanikio, hali hii pia huwakuta hata baadhi ya viongozi wa timu au vyama vya michezo ambao wanapokua na nia ya kugombea au kuteuliwa nafasi fulani, uteuzi wake huzungukwa na changamoto ya kutokubalika kwa sababu ya historia au rekodi zake mbaya za nyuma.

Kimsingi, mchezaji au mtu yoyote ambaye anahakikisha anafanya majukumu yake kwa kuzingatia nidhamu, sheria na kanuni, mara nyingi hupata matokeo chanya na faida yake huiona ndani ya muda mfupi.

Kwa wana michezo, wakati huu wa lala salama ni muda mzuri wa kuzidisha nidhamu kwa ajili ya kusafisha 'mabaya' yote ya nyuma na hatimaye kujifungulia 'neema' mpya kuelekea msimu mpya.

Ushauri huu unawahusu wanamichezo wote, leo hii moja ya sifa iliyomfikisha mshambuliaji tegemeo wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta katika kikosi cha Aston Villa ni nidhamu binafsi. Inawezekana endapo kila mchezaji au kiongozi atajitambua na kufanya majukumu yake kwa weledi.

-

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kikulacho ki nguoni mwako



Na Barnabas Maro

"KIKULACHO huwa ndani ya nguo iliyo mwilini mwako." Twakumbushwa kuwa mtu anayeweza kutudhuru ni yule anayetufahamu vizuri.

Aidha husemwa "Adui wa mtu ni mtu." Kwamba binadamu huathiriwa na binadamu mwenzake. Hii ni methali ya kutukumbusha kuwa aghalabu matatizo tuyapatayo husababishwa na watu tunaoishi nao kila siku.

Damka/rauka kisha nenda kakae mkabala (tazamana) na klabu ya Simba au Yanga. Hapa utaona watu wa makundi mawili. Moja ni la muuza kahawa na la pili wanaelezana na kubishana kuhusu ubora na udhaifu wa timu.

Kundi hili ambalo hakuna yeyote aliyecheza kandanda, husimama mduara wakimzingira msemaji anayezungumza mithili ya chiriku!

Yanayozungumzwa hapo ni kuwasifu baadhi ya wachezaji na kuwasema vibaya wengine. Aidha huwasema viongozi wasiofaa na kuwasifu wengine wanaojali masilahi ya vilabu na wachezaji.

Kati ya pande zote mbili, wapo wanachama na wasio wanachama, yaani wanaofuata upepo. Watu wa aina hii huwa upande wa timu yenye mafanikio dhidi ya timu zingine, hasa hizi ziitwazo 'watani wa jadi' ingawa si watani ila ni mahasimu!

Idadi kubwa ya kundi hilo ni wale wanaofuata timu inayoshinda mara kwa mara na kuikimbia inayoshindwa. Hawa si wanachama ila ni mashabiki wanaofuata upepo kama bendera. Miongoni mwao hupenda timu kwa kuvutiwa na wachezaji fulani, kocha, wafadhili na baadhi ya viongozi.

Wanaowafuata viongozi ni wale wanaopewa nafasi za kuwa walinzi na kuitwa 'makomando.' Katika hali halisi komando ni kundi la askari wa jeshi kwa kazi maalum.

Eti wao hujiona bora kuliko wanachama wanaojitoa kwa hali na mali! Kwa hali hiyo, vilabu vitakuwa vikiwaneemesha baadhi ya viongozi na 'makomando' wao na kuvifanya kuwa tegemezi kwa miaka kadhaa.

'Mfadhili' ni mtu anayemfanyia wema mtu mwingine; mtu au taasisi inayosaidia mtu au jamii kwa fedha au vifaa kwa ajili ya kuendeshea mradi.

Yanga na Simba zimekuwa na wafadhili mbalimbali lakini ziko vilevile bila maendeleo ya maana. Zimebaki kuwa 'omba omba' mwaka hata mwaka kiasi cha kuwachosha wafadhili wao.

Kungekuwa na uangalizi makini, wallahi leo Yanga na Simba zingekuwa na maendeleo makubwa ya kuigwa na nchi jirani, kama Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Malawi lakini wajanja (nadhani tuwaite wezi) ndio wanaojinufaisha!

Baadhi ya wanachama hugombea nafasi za uongozi ili kujinufaisha badala ya kuzijenga Simba na Yanga zilizoundwa miaka kadhaa iliyopita. Yanga ilizaliwa mwaka 1935 ilhali Simba mwaka 1936 baada ya kutengana.

Nani aliyesikia mchezaji wa Azam FC akilalamika kwa kucheleweshewa fedha za usajili au kutolipwa mshahara wake kila mwezi? Ni timu pekee yenye viwanja vyake, gymnasium/gym yaani ukumbi wa michezo ya mazoezi ya viungo, zahanati na mambo muhimu yanayohusu afya ya wachezaji.

Tujiulize: Asingetokea MO Dewji, leo Simba ingekuwa hali gani? Hata huyu naye kuna wakati alitangaza kujitoa lakini baada ya kuombwa sana na baadhi ya viongozi wa ... (nachelea kuweka wazi) akakubali kurejea kundini.

Sasa alhamdulillahi (tamko la kuonesha shukrani kwa Mwenyezi Mungu) mambo yanakwenda kisasa.

Kadhalika Yanga isingekuwa na udhamini wa GSM ingekuwaje? Kumbuka jinsi ilivyoitwa 'omba omba' iliposaidiwa na aliyekuwa kocha wao Mkongomani Mwinyi Zahera! Sasa Yanga wanapumua baada ya kampuni ya GSM kuingia 'kundini' na kuwafanya wawe na sauti mbele ya wale jamaa ... (msomaji nakuachia ujaze mwenyewe.)

Kuna mtu aliyeona mbele akataka kuifanya Yanga iwe ya kimataifa na kujitegemea, lakini alipoona haielekei na hata kutumiwa 'makomando' wamtukane yeye na familia yake, akawaachia klabu yao.

Mtu huyo hayupo nasi sasa kwani ametutangulia mbele ya haki. Mungu amrehemu.

Wahenga walisema: "Ushikwapo shikamana (ukichwewa na jua lala)." Maana yake unaposhikwa na mtu shikamana au nawe jitahidi. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu aliyepatwa na tatizo kisha akapata mtu wa kumsaidia. Humhimiza ajikakamKadhalika yasemwa: "Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi." Maana yake usijivune kwa kwenda mbele, unaweza kurudi nyuma wakati wowote.

Ngoja niwapooze: "Kujikwaa si kuanguka bali ni kwenda mbele." Mtu anapojikwaa huwa si kwamba ameanguka ila huenda mbele. Hii ni methali ya kutumiwa katika muktadha ambapo mtu amekabiliana na tatizo fulani anapotenda jambo. Huweza kumhimiza asikate tamaa au asife moyo bali aendelee.

Yanga, Simba mpo?

Methali: Kukataa kwa chungu ni kuvuja.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Ripoti yabaini watoto wenye ulemavu kukosa elimu awali

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya HakiElimu imezindua ripoti mbili zinazoangazia makuzi ya mtoto, ulinzi na maendeleo ya elimu ya awali nchini, huku ikionyesha kuwa bado kuna changamoto ya uandikishwaji wa watoto wenye ulemavu na wanaoishi katika mazingira magumu katika elimu hiyo ya awali.

Akizungumza katika uzinduzi wa ripoti hiyo uliofanyika kwa njia ya mtandao, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kalage, alisema pamoja na mafanikio ambayo nchi imeyafikia katika elimu ya awali, changamoto kubwa imebaki kwa kundi hilo.

"Sheria ya mtoto ya mwaka 2008 na sera ya elimu ya mwaka 2014, zinatoa haki kwa kila mtoto kupata elimu ikiwamo elimu ya awali ambayo ni ya lazima. Sheria hizi zinaweka wajibu kwa mzazi, mlezi na jamii kuhakikisha mtoto anapata elimu ya awali kabla ya kujiunga na elimu msingi,"alisema Dk. Kalage na kuongeza:

"Kwa miongozo hii, kila shule ya msingi Tanzania ina angalau darasa la awali. Kwa mfano, kuna madarasa ya awali 17,493 sawa na asilimia 99.6 ya shule za msingi 17,562 za umma na zisizo za umma zilizopo kwa sasa. Hali ya uandikishaji watoto katika madarasa ya awali siyo mbaya ukilinganisha na malengo yaliyowekwa."

Alisema katika wilaya ambako tafiti zilifanyika, wastani wa uandikishaji wa elimu ya awali ikilinganishwa na matarajio ni zaidi ya asilimia 100.

"Changamoto ya uandikishaji inabaki kwa makundi ya watoto wenye ulemavu na wanaoishi katika mazingira magumu na jamii za wafugaji ambako wastani wa uandikishaji umebaki kuwa chini ya asilimia 70 ya malengo ya uandikishaji," alisema Dk. Kalage.

Pia, changamoto nyingine waliyoibaini katika utafiti huo ni pamoja na kukosekana kwa mazingira mazuri ya kujifunzia na kufundishia kwa watoto wa madarasa hayo ya awali.

Alisema asilimia 100 ya wilaya zilizofanyiwa utafiti huo zilionyesha kuwapo na uhaba wa miundombinu bora ya vyoo, madarasa, majisafi, lishe bora shuleni, madawati na mahali salama pa kuchezea watoto, vifaa vya michezo, uhaba wa walimu wenye sifa ya kufundisha madarasa hayo pamoja na uelewa mdogo wa mbinu za kufundishia

"Mathalani, katika shule zote zilizohusika kwenye utafiti hakukuwa na walimu wenye mafunzo maalumu kwa ajili ya kufundisha madarasa ya awali. Hii ina maanisha kuwa katika shule hizo walimu waliokuwa wakifundisha madarasa ya awali hawakuwa na sifa stahili ya kufundisha madarasa hayo," alisema Dk. Kalage.

Alisema asilimia 52.6 ya walimu wa madarasa ya awali walioshiriki katika utafiti huo walioonyesha kutokuwa na uelewa sahihi wa maana ya elimu ya awali na mahitaji yake.

"Hali hii imesababisha ufundishaji na malezi ya watoto wa awali shuleni kufanana kwa kushabihiana na ile ya watoto wa shule ya msingi. Asilimia 50 ya walimu walioshiriki katika tafiti hizi, walitoa adhabu kali kama za viboko na vitisho ili kuhakikisha watoto wanakuwa na nidhamu. Mbinu hizi hazipendekezwi kutumika kwa watoto wa shule za awali," alisema Dk. Kalage.

Alisema utafiti huo ulibaini changamoto ya ushirikiano mdogo kati ya wazazi na walimu katika kuhakikisha mtoto anapata malezi na elimu stahili inayoendana na umri na mahitaji yake.



Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, mkoani Tabora, Peres Magiri akizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Sikonge wafikisha 81% utoaji mikopo

**Na Tiganya Vincent, SIKONGE**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Sikonge imepongezwa kwa kufikisha asilimia 81 ya uchangiaji wa asilimia kumi ya fedha zinazotokana na mapato ya ndani kwenye mifuko ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, wakati akitoa salamu za Mkoa katika kikao cha robo ya tatu cha Baraza la Madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo.

Alisema hadi kufikia mwezi Machi, jumla ya Shilingi milioni 125 zimetolewa kwa walengwa hao, wanawake wakikopeshwa Sh. milioni 78, vijana milioni 40 na wenye ulemavu milioni saba.

Alisema kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2019 zimeelekeza mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu wa kutenga fedha asilimia kumi ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye vyanzo vya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vilivyo sajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Makungu alisisiiza katika kipindi kilichochabaki wamehakikisha wanakamilisha asilimia 19 zilizobaki katika utoaji wa mikopo hiyo.

Pia, aliuagiza uongozi kuhakikisha fedha za mikopo Sh. milioni 167.2 ambazo haijarejeshwa zifuatiliwe ili zirejeshwe.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. milioni 106.5 wadaiwa wanawake, milioni 55.5 wanadaiwa vikundi vya vijana na walemavu wanadaiwa Sh. milioni 5.1.

Katika hatua nyingine, ameuagiza uongozi wa halmashauri hiyo kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kuwa bado wako chini ya lengo la kitaifa ya zaidi ya asilimia 80.

Alisema hadi Machi walikuwa wamekusanya Sh. bilioni 1.7 ya lengo kukusanya kiasi cha bilioni 2.8 ambayo ni sawa na asilimia 61.

Alisema serikali iliweka wazi kuwa halmashauri ambayo itashindwa kufikia lengo, Mkurugenzi Mtendaji na Mweka Hazina wake watachukuliwa hatua.

Pia, alisisitiza ni vyema wakatumia muda uliobaki kumaliza mwaka wa fedha huu kuhakikisha wanazidi lengo la kitaifa la ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Makungu alisema njia pekee ya kuhakikisha wanadhibiti upotevu wa mapato kwa kutumia mashine za kielekironiki katika maeneo ya ukusanyaji na mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mtandao katika vituo vya kutolea huduma kama vile hospitali hadi zahanati.

# Tumbaku yote Urambo kununuliwa

**Na Lucas Raphael, TABORA**

KAMPUNI ya ununuzi wa tumbaku ya Alliance One imekubali kununua kilo 705,474 za tumbaku ya msimu uliopita ya vyama 10 vya ushirika (AMCOS), wilayani Urambo, mkoani hapa.

Hayo yamebainishwa jana na Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wilayani humo, Absama Kajuna alipokuwa akitoa taarifa ya maendeleo ya zao hilo katika mkutano wa wadau wa kilimo.

Alisema tumbaku hiyo maarufu kama makinikia, sasa itanunuliwa kwa bei ya Sh. 1,265 sawa na dola za kimarekani 0.55 kwa kila kilo moja, jumla Sh. 892,474,610.

"Nafurahi kuwajulisha kuwa tumbaku yote iliyokosa soko mwaka jana ya vyama 10 vya msingi sasa itanunuliwa na kampuni ya Alliance One, ila haitakuwa na madaraja, itachukuliwa kwa bei moja tu," alisema.

Mkuu wa wilaya hiyo, Angelina Kwingwa, alibainisha kuwa kitendo cha kuchelewa kwa ununuzi ya zao hilo mwaka jana, kilichangia tumbaku hiyo kutonunuliwa yote jambo ambalo limewasababishia hasara wakulima.

Alisema upungufu uliojitokeza mwaka jana kwa kampuni ya Magesa kuwa imekosa usafiri wa kubebea tumbaku yote wakati mkataba ulikuwa umeshafungwa hayakubaliki.

Alisisitiza kuwa mkataba wa ununuzi ukishafungwa masuala ya usafiri sio jukumu la mkulima ni juu ya mnunuzi mwenyewe na kuonya kitendo hicho kikijirudia kampuni itawajibika kwa hasara itakayotokea.

Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya hiyo, Adam Malunkwi, alisema kama kampuni hiyo imekubali kununua tumbaku hiyo iliyosalia msimu uliopita, waichukue mara moja badala ya kuiacha kwenye maghala.

Alisisitiza kuwa kuanzia sasa Bodi ya Tumbaku Tanzania haitatoa leseni kwa kampuni yoyote ya ununuzi ambayo haitakuwa imekidhi vigezo.

Kaimu Mkurungezi wa Bodi hiyo, Stanley Mnozya, alisema kwamba kutokana na ununuzi huo, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo itapata ushuru wa Sh. 26,774,238 na vyama vya msingi kupitia chama kikuu cha wakulima kitapata Sh. 44,621,230.

Alisema ununuzi huo umesaidia wakulima wa tumbaku kupata pesa kwa kuwa bila jitiada za bodi hiyo kufanya ushawishi tumbaku hiyo ili kuwa iendelea kubaki kwa wakulima kitu ambacho kingesababisha kutupwa.

Aliwataka wakulima wenye tumbaku ndani wazipelekea kwenye magahala ili ziweze kununuliwa kwa kuwa hadi sasa kampuni ya ununuzi wa tumbaku zinahitaji tumbaku hizo za msimu ulipita.

# RC Mwanza atoa siku 14 mil. 432/- makusanyo zirudishwe

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ametoa siku 14 kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Misungwi, kuwakamata na kuwachukulia hatua kali baadhi ya watendaji waliofanya hujuma ya wizi wa Sh. milioni 432 za makusanyo ya halmashauri na kurejeshwa kabla ya Juni 30, mwaka huu pamoja na mashine za kukusanyia mapato tatu zilizopotea.

Mongella alito agizo hilo jana wakati akizungumza katika Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo la kujadili hoja za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2018/2019 na kubainishwa upotevu wa mashine tatu katika mazingira ya kutatanisha.

Alisema kiasi cha fedha ambacho hakikuingizwa kwenye mfumo wa serikali na kuibiwa kirejeshwe kwa kipindi cha muda huo aliotoa.

Alisema haiwezekani mtu anaamka asubuhi na kukusanya fedha mbichi ambazo wanakula kabla hawajapeleka benki na kutaka fedha hiyo irudishwe, mashine za kieletroniki za kukusanyia mapato walizonunua 97 kati ya hizo 26 hazitumiki huku tatu zikiwa zimepotea, zirejeshwe ndani ya wiki mbili na ziwe zimefika katika ofisi yake.

"Hakuna utaratibu wa kupeana majibu rahisi rahisi asiporejesha tutampeleka mahakamani na kutengeneza utaratibu wa kumtoa kazini," alisema Mongella.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi Antonty Masele, alilaani vitendo hivyo na kudai vinarudisha nyuma juhudi za serikali katika ukusanyaji wa mapato kwa kuwa aliyoyasema Mkuu wa Mkoa ni sahihi hivyo watahakikisha waliohusika na mambo hayo wanachukuliwa hatua ili waweze kurejesha na hesabu zote ziingie kwenye mfuko wa serikali ziwasaidie wananchi.

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Misungwi, Kambadu Samweli, aliomba serikali kuwachukuliwa hatua na maelekezo yaliyotolewa na mkuu huyo yafuatwe kwa kuwa serikali haikubaliani na upotevu huo.

Hoja ya wizi huo wa Sh. milioni 432 iliibuliwa na ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati wa Baraza la kujadili hoja za CAG kwa mwaka 2018/2019.



Wafanyabiashara wa chupa tupu za plastiki, wakipakia kwenye gari kwa ajili ya kuzipeleka sokoni Buguruni Dar es Salaam jana, kwaajili ya kuziuza ili wajipatie riziki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# AIC yato fursa kujiunga kilimobiashara

**Na Maulid Mmbaga**

KITUO cha Ubunifu wa Kilimobiashara (AIC), Idara ya Taasisi ya Pass, kimetoa fursa kwa vijana wenye nia ya kujiunga na kilimo hicho.

Taarifa hiyo imetolewa kwenye tovuti ya kituo hicho ambayo inaeleza upokeaji maombi ya kujiunga na vituo Atamizi vya kilimobiashara vilivyopo SUA, Morogoro na Taliri Fam, Mbende Kongwa, mkoani Dodoma.

Taarifa hiyo ilisema katika vituo tajwa AIC itawapa fursa vijana ya kuanzisha, kumiliki na kuendesha kilimobiashara katika sekta ndogo ya mboga, matunda, mifugo na nyama.

Ilisema wanahitajika vijana watiifu na wenye fikra chanya na watakaoshiriki watapewa vifaa, miundombinu, malighafi na mtaji wa kufanya kilimobiashara na watausimamia kwa kipindi cha miezi 12.

"Katika kipindi chote watahiniwa watapewa usimamizi wa karibu ikiwamo ushauri wa kibiashara na upelembaji, ili kuhakikisha wanafanikiwa katika shughuli zao za kilimobiashara.

"Baada ya muda huo kukamilika, vijana watakaofanikiwa kwenye kilimobiashara, AIC itawawezesha kuanzisha biashara kama hiyo kwenye maeneo yao," taarifa hiyo ilisema.

Iliongeza kuwa vijana wenye nia watume maombi ya kujiunga katika kituo kimojawapo SUA-AIC, Morogoro kinachojihusisha na mboga na matunda au AIC, Kongwa Taliri Fam (PRC) Mbande, unenepeshaji, ufugaji Mbuzi na usindikaji wa nyama.

Pia vijana 280 watachaguliwa kwenye awamu ya kwanza, 200 kituo cha Morogoro na 80 cha Kongwa na Oktoba 2020 itakuwa ni awamu ya pili 140, Morogoro watachaguliwa 100 na Kongwa 40.

## Baba adaiwa kumpaka mlenda mtoto wa kambo na kumbaka

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MWANAMUME ambaye hakutajwa jina lake kwa sababu za kiuchunguzi, wilayani Shinyanga, anadaiwa kumbaka mtoto wake wa kambo mwenye umri wa miaka sita kwa kumpaka mboga yenye utelezi (mlenda) sehemu za siri na kumwingilia kimwili.

Ofisa Tarafa ya Samuye, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Ntarle Magese, alitoa madai hayo wakati akitoa elimu ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, kwa waelimishaji rika Kata ya Mwamala kwa kushirikiana na Shirika la Agape, na elimu ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Alisema ndani ya jamii kumekuwapo na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia, na kudai viongozi wa kijiji kusuasua kuyashughulikia likiwamo suala la mwanamume wa kijiji cha Ibanza, kumbaka mtoto wake wa kambo kila mara, kwa kumpaka mlenda.

"Tuhuma hizi bado tunazifanyia uchunguzi, mtoto ameshahojiwa na kukiri huwa anaingiliwa na baba yake huyo wa kambo kimwili mara kwa mara, na kupakwa mboga yenye utelezi mlenda sehemu zake za siri na kisha kupenyezewa uume na kufanya naye ngono," alidai Magese.

"Kutokana na kuendelea kuwapo na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia, yakiwamo ya ubakaji, mimba za wanafunzi, kutelekeza watoto, vipigo kwa wanawake hadi kuharibu ujauzito, naombeni sana viongozi wa vijiji acheni kuyafumbia matukio haya, bali yachukulieni hatua ili jamii ibaki kuwa salama,"aliongeza.

Mkurugenzi wa Shirika la Agape mkoani Shinyanga, linalotetea haki za wanawake na watoto, John Myola, alisema katika kipindi hiki cha likizo wanafunzi wakiwa nyumbani muda mrefu, jamii imejisahau na kuwafanyia vitendo vya ukatili watoto hao.

Alisema baada ya kuligundua hilo, ilibidi waanzishe utoaji wa elimu ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona, pamoja na kutoa msaada wa vifaa kinga zikiwamo sabuni na ndoo za majitiririka, huku wakitoa elimu ya kupinga vitendo vya ukatili kipindi hiki wanafunzi wakiwa nyumbani likizo kuwalinda.

HABARI DODOMA

# 'Ni aibu ofisi za serikali kutumia maziwa ya kopo'

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameziasa ofisi za serikali na wadau mbalimbali nchini, kutumia maziwa yanayozalishwa kupitia mifugo ya nchini badala ya kutumia ya kopo kutoka nchi za nje.

Ulega, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa, wakati akifungua maadhimisho ya Wiki ya Maziwa yaliyofanyika kitaifa mkoani Dodoma huku kilele cha maadhimisho hayo kikitarajiwa kufanyika Juni mosi, mwaka huu.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, unywaji wa maziwa yanayozalishwa nchini kutasaidia kuchochea na kuongeza uchumi wa taifa na kwa mwananchi mmoja mmoja.

"Ni aibu kubwa kwa ofisi za serikali kutumia maziwa ya kopo, nasema hivi kwa sababu hivi leo ukiingia katika ofisi za serikali utakuta maziwa ya kopo ndio yanatumika, kwa nini tusitumie maziwa yetu," alihoji Ulega.

Aliwataka wananchi kupenda na kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuzipatia soko yakiwamo maziwa ili kukuza uchumi wa nchi.

Pia, Ulega alisema takwimu zinaonyesha kuwa taifa liko chini katika suala la unywaji wa maziwa duniani kwa mwaka mtu mmoja anakunywa lita 54, wakati anatakiwa kunywa angalau lita 200.

Alifafanua kuwa kikanda takwimu zinaonyesha mtu mmoja anatakiwa kunywa lita 74 kwa mwaka wakati Tanzania upo uwezekano wa kuzalisha lita bilioni tatu kwa mwaka.

"Tanzania tuna uwezo wa kuzalisha lita bilioni tatu, kwa mwaka, lakini licha ya kuzalisha maziwa mengi na kuongoza kwa kuwa na mifugo mingi, lakini bado Watanzania wameonekana kuwa wavivu wa kunywa maziwa na wengine kuonekana kupendelea kunywa maziwa ya unga yanayozalishwa nchi za nje, hii ni aibu sana tuwe wazalendo Watanzania,"alisisitiza Ulega

Alisema, kama unywaji wa maziwa utazingatiwa ipasavyo kwa Watanzania wote uchumi wa viwanda na taifa kwa ujumla utaongezeka.

Alisema sekta ya maziwa, ni wezeshi kwa uchumi wa Taifa la Tanzania na hivyo jitihada zinatakiwa kufanyika kuhakikisha unywaji wa maziwa unazingatiwa kwa Watanzania wote.

Kwa upande wake Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa, Dk. Sophia Mlote alisema, bodi hiyo imefanya mapitio ya sheria ya maziwa ya mwaka 2004, ili kuendana na kasi ya mahitaji ya sasa kwa lengo la kuwezesha Bodi ya maziwa kuchochea maendeleo katika mnyororo wa thamani.

Hata hivyo, alisema bodi hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya ukusanyaji na usafirishaji bidhaa hiyo.



Mmoja wa wenye ulemavu waliohitimu mafunzo ya udereva wa Bajaj, Wema Hassani, akisoma risala katika hafla ya kuhitimu mafunzo hayo, iliyofanyika jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Shule zajipanga wanafunzi kusoma kwa awamu

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

BAADHI ya shule na vyuo mkoani Dodoma, zimebainisha mikakati mbalimbali kwa ajili ya kukabiliana na virusi vya ugonjwa wa corona, wanafunzi watakaporudi shuleni, ikiwa ni pamoja na kusoma kwa awamu.

Mikakati mingine ni pamoja na wanapoingia madarasani kufanya mitihani wanaingia asubuhi hadi mchana na yasiyo ya mitihani watakuwa wanaingia mchana hadi jioni, ili kuepuka msongamano.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Dabalo, Wilaya ya Chamwoni, mkoani Dodoma, Vicent Stephano, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, namna bora wanafunzi hao kusoma kwa awamu ili kuepusha idadi kubwa katika darasa moja.

Alisema shule hiyo ina vyumba vya madarasa vinne, idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na wanafunzi na kutoa mfano kidato cha kwanza kina wanafunzi 190.

"Vyumba vya madarasa ni vichache ukilinganisha na idadi ya wanafunzi, kwa kuwa ni lazima darasani kuwe na nafasi ya kutosha kati ya mwanafunzi na mwenzie, tunapanga wanafunzi hao wasome kwa zamu ili tuwatawanye kwenye madarasa yote," alisema.

Utaratibu mwingine walioweka ni kuvuta maji ya bomba katika shule hiyo ili kurahisisha unawaji mikono wa wanafunzi pamoja na walimu.

Alisema kila chumba cha darasa kitakuwa na ndoo ya maji yanayotiririka kwa ajili ya wanafunzi kunawa mikono kabla ya kuingia darasani huku wakiwahamasisha wazazi kuwanunulia watoto wao barakoa.

Makamu Mkuu wa Chuo cha Afya cha Decca, anayeshughulikia fedha na mipango, Dotto Gombo, alisema kabla ya vyuo kufungwa walichukua tahadhari zote ikiwa ni pamoja na kuunda timu maalum kwa ajili ya ufuatiliaji na udhibiti wa corona.

Gombo, alisema katika tawi lao la chuo la Nala jijini hapo wana kituo cha huduma ya kwanza kwa wanafunzi, vifaa vya kunawia mikono, wanazalisha vitakasa mikono pamoja na kuwa na vifaa vya kupima joto.

Alisema kila mwanafunzi atakayeingia chuoni au darasani ni lazima apimwe joto na akibainika kuwa lipo juu watamtenga katika eneo maalum.

"Tuna timu ya ufuatiliaji na udhibiti wa corona katika maeneo ya huduma, tuna vifaa vyote vinavyotakiwa katika sehemu zote za kutolea huduma, pia tunazalisha barakoa katika kiwanda chetu kwa ajili ya wanafunzi, niwatake wanafunzi kutokuwa na wasiwasi pindi watakaporudi chuoni kwa kuwa tumejipanga," alisema Gombo.

# Bahi yaelimisha wananchi kujikinga corona

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma, imetoa elimu ya kujikinga na ugonjwa wa corona nyumba kwa nyumba kwenye vijiji 32, vya wilaya hiyo ili kuwawezesha wananchi kujikinga.

Elimu hiyo inatolewa na halmashauri ya wilaya hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya chini ya ufadhili wa Shirika la World Vision, lengo likiwa ni kuwakinga wananchi na maambukizo ya ugonjwa huo.

Akizungumza na wananchi kwenye Kijiji cha Msisi, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Paulina Landa, alisema ni wajibu wa kila mmoja kujikinga na ugonjwa wa corona kwa kufuata taratibu zote zinazotolewa na wataalam wa afya.

Landa, alisema ingawa hakuna mgonjwa mwenye maambukizo katika wilaya hiyo, wameamua kutoa elimu ya kujikinga kwa kuwa wilaya hiyo ni barabara kuu ya magari yanayokwenda nje ya nchi.

"Wananchi wetu wengi wanafanya biashara kwenye magari yanayokwenda mikoa ya jirani na nje ya nchi kwa sababu hapa ni barabara kuu hivyo ni lazima tuwaeleweshe jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo wanapokuwa kwenye shughuli zao za kila siku."

"Tumekuwa tukitoa matangazo kwa njia ya magari yanayozunguka mitaani kwa ajili ya kujikinga na corona, lakini watu wengi walikuwa hawapati hiyo elimu na ndiyo maana tumeamua kutoa elimu nyumba kwa nyumba," alisema Landa.

Kwa upande wake mtaalamu wa masuala ya afya na lishe kutoka Shirika la World Vision Tanzania, Dk. Salome Mtango, alisema njia pekee ya kujikinga na ugonjwa wa corona ni kuzingatia kanuni za afya zinazotolewa na wataalam kwa kuwa hauna tiba.

Steven Lucas, alisema kuwa mara nyingi walikuwa wakisikia tahadhari za kujikinga na ugonjwa wa corona kwenye vyombo vya habari pamoja na matangazo yanayopita kwenye kijiji chao, lakini walikuwa hawaelewi.

"Leo nawapongeza kwa sababu mmefika nyumbani kwangu mmenikuta na mke wangu na watoto wangu, mmezungumza na sisi, tumewauliza maswali yaliyokuwa yanatusumbua kuhusu huu ugonjwa wa corona, sasa tunaweza kujikinga kwa tahadhari kubwa,"alisema.

HABARI ZANZIBAR

# Wakulima watakiwa kuwekeza kwenye viungo

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Biashara na Viwanda imewataka wakulima kuwekeza katika kilimo cha mazao ya viungo ambayo soko lake lipo la uhakika ndani na nje ya nchi.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, alisema mahitaji ya mazao ya viungo ni makubwa ulimwenguni pamoja na ya ndani kwa viwanda viwili vya mafuta ya mimea pamoja na makonyo.

Aliyataja mafuta ya mimea yanayotarajiwa kuzalishwa kuwa ni mkaratusi, mchaichai, mrehani na mdalasini.

Alisema ukarabati mkubwa uliofanywa katika kiwanda cha makonyo, Wawi Pemba, sasa kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 300 za mafuta ya makonyo yanayotokana na uzalishaji wa karafuu.

Kadhalika, alisema katika kiwanda kipya cha Mgelema kilichopo Pemba, ambacho ni mkopo kutoka kwa kampuni ya INDESSO ya Indonesia, mahitaji yake katika uzalishaji wa mafuta ya mimea ni tani 300 kwa mwaka.

"Mheshimiwa Spika wakati umefika sasa wakulima wetu wajikite katika kilimo cha biashara ya mazao ya viungo ambacho soko lake lipo la uhakika ndani na nje ya nchi," alisema.

Alisema Wizara ya Biashara na Viwanda, kazi kubwa wanayoifanya sasa ni kuwahamasisha wananchi kuanzia vikundi vya ushirika na mabaraza ya vijana kuanzisha mashamba ya kilimo cha viungo.

Wizara ipo katika hatua za mwisho kuanza kilimo cha mkaratusi katika mashamba ya Chamanagwe pamoja na Micheweni, Mkoa wa Kaskazini ambayo yatatumiwa kuotesha mikaratusi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya viwanda vyake viwili viliopo Pemba.

"Mheshimiwa Spika wizara imejipanga kuimarisha maeneo ya mashamba yake yaliopo Chamanangwe na Micheweni Pemba, kwa ajili ya kuotesha mikaratusi ili iweze kukidhi mahitaji ya kuendesha viwanda viwili vilivyopo Pemba kupata malighafi," alisema.

Zanzibar katika miaka ya 1960-70 ilikuwa ikiongoza kwa uzalishaji wa mazao ya viungo, pilipili manga na pilipili hoho pamoja na uzalishaji wa mafuta ya nazi yanayotokana na mbata na kusafirisha nje ya nchi.



Mawaziri wasio na Wizara Maalum, Juma Ali Khatib (kushoto) na Said Soud, wakibadilishana mawazo nje ya kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ujenzi kiwanda kuongeza thamani mwani mbioni

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema mchakato yakinifu kuhusu ujenzi wa kiwanda cha kuongeza thamani na kusarifu Mwani na bidhaa nyingine umeanza huko Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiwasilisha makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2021 huko Chukwani mjini Unguja.

Alisema mazungumzo kuhusu ujenzi wa kiwanda cha kusarifu bidhaa za mwani umefikia hatua nzuri kwa ushirikiano ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wawekezaji kutoka Indonesia.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba juhudi za kuanzisha kiwanda ambacho kitasaidia kusarifu mwani kwa ajili ya kuongeza thamani na ubora wake kwa wakulima mchakato wake unaendelea vizuri...tunatarajia kiwanda kitajengwa Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba," alisema.

Alisema malengo ya Serikali ya Zanzibar ni kuona wakulima wa zao la mwani wanapata mafanikio makubwa ya kupiga hatua kubwa za kiuchumi kwa kupata soko la bidhaa zao kutokana na kuongezeka thamani ya matumizi mengi kwa wakati mmoja.

Alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi ya tatu katika Bara la Afrika inayozalisha mwani kwa wingi na kusafirishwa katika nchi za Ulaya hadi Asia ikiwamo Indonesia.

Aliwapongeza wanawake walio katika maeneo ya mwambao wa pwani ya Unguja na Pemba kwa kuitikia na kujikita katika kilimo hicho ambacho kimeleta mabadiliko makubwa ya maisha ya wakulima na kuacha utegemezi kutoka kwa waume zao.

Aliwataka wakulima wa mwani kubadilika na kutuma teknolojia ya kisasa ikiwamo aina ya mbegu bora zinazokubalika na kuhimili matatizo mbalimbali ikiwamo maradhi.

Alisema wakulima wa mwani wa Pemba wamepiga hatua kubwa ya uzalishaji wa zao hilo wenye sifa unaoweza kuingia katika soko la kimataifa.

"Tunataka kuona wakulima wa zao la mwani wanapiga hatua kubwa ya uzalishaji wa kilimo hicho na kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwa kujenga kiwanda kitakachosarifu na kuongeza thamani ya mwani," alisema.

Balozi Amina aliliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha jumla ya Sh. 23,569,700,000 kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020-2012.

# SMZ kuunda kikosi doria wahujumu rasilimali

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inakusudia kuunda kikosi cha doria kwa ajili ya kupambana na watu wanaofanya hujuma katika matumizi ya rasilimali ikiwamo misitu na mchanga.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, wakati akijibu hoja za wajumbe waliochangia bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020-2012.

Alisema wizara ipo katika hatua za mwisho za kufanya mashauriano na vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu kuanzishwa kwa doria yenye lengo la kudhibiti uharibifu wa rasilimali za taifa.

Alisema kikosi cha doria kinahitajika kwa sababu hivi sasa watu wamekuwa wakivamia maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuchota mchanga nyakati za usiku na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

"Tumepokea malalamiko yapo baadhi ya maeneo ikiwamo mashamba ya wananchi yanavamiwa usiku na kuchimbwa mchanga," alisema.

Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliishauri serikali kuunda kikosi ambacho kitafanya doria kudhibiti uharibifu wa mazingira ikiwamo wananchi kuvamia misitu ya hifadhi.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara maalumu ya vikosi vya SMZ, Haji Omar Kheir, alisema uharibifu wa mazingira ikiwamo uchotaji wa mchanga katika maeneo ambayo hayaruhusiwi ni moja ya changamoto kubwa iliyojitokeza sehemu mbalimbali ikiwamo mjini hadi vijijini.

Alikiri kuwapo kwa uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya mawe na kokotoa yaliopo Kibele na Kidimni kwa watu binafsi kufanya shughuli hizo kinyume na sheria.

"Serikali haina pingamizi kuhusu suala la kuwapo kwa doria za maeneo ya hifadhi ya rasilimali za taifa ikiwamo misitu ya hifadhi hadi maeneo yenye uhifadhi wa mchanga na mawe," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio na mapato ya bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020-2021, jumla ya Sh. bilioni 129.86 zitatumika kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo.



MJENGO WA KHLOE KARDASHIAN SOKONI Uk. 14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI MEI 30, 2020



## LULU JAMANI!

# Umri wake mdogo, mambo mazito

MWIGIZAJI nyota wa Bongo Muvi, Elizabeth Michael, maarufu kama Lulu, ameibua mjadala baada ya kutoboa kwamba umri wake mdogo mambo yake makubwa na hata mchumba wake anajua jambo hilo.

Akizungumza katika kipindi cha Salama kinachorushwa na East Africa TV, Lulu amesema kwamba hana matatizo katika uhusiano wake kutokana na kila kitu kinachotakiwa kufanywa na mwanamke anakijua.

Hata hivyo, amesema mchumba wake DJ Majizo, ameridhika na umri wake mdogo lakini ana nafsi kubwa ndiyo inamfanya waendelee kuishi kwa furaha hadi sasa.

"Katika uhusiano umri sio jambo la kuzingatiwa, kwanu nina umri mdogo lakini nafsi yangu kubwa na hata yeye ninayeishi naye anajua hilo," amesema Lulu.

Amesema wakati mwingine kuna baadhi ya watu wanataka kumuharibia kutokana na chuki zao, kuna wakati walimzushia kila mwanamume anayetoka naye anakufa ghafla.

"Unajua kila ninapopima idadi ya wanaume niliokuwa nao sio wote wamefariki kama walivyonizushia, mbona kuna wengine wapo hai?..Kuna watu wanamchukia mtu na wanapenda kuniumiza," ameongeza kusema.

Akijibu tuhuma za kuiba mwanaume wa mtu ambaye anaendelea kuishi naye, Lulu amesema jambo hilo hakuna, kwani yeye na Majizo wametoka mbali.

"Mchumba wangu nimemfahamu miaka mingi kidogo wakati napenda sana club na yeye alikuwa Dj katika hiyo club, tulikuwa tuna urafiki, tunajuana na hata kwenye uhusiano kuanza haikuwa ngumu, japo nilimkuta ametoka kuwa kwenye mapenzi na mwanamke mwingine na alinihakikishiwa kwamba yameisha, amesema Lulu.

BASI SAWA

## Barnaba asimulia alivyoepuka mihemko

MWANAMUZIKI pendwa wa Bongo Fleva, Barnaba, amesema ndoto yake ya kuwa msanii mkubwa wa muziki hapa nchini, imefanikiwa baada ya kupitia changamoto nyingi, ikiwamo kukabiliana na matamanio ya ujana.

Barnaba, amesema kwa kawaida katika kipindi cha kubalehe, vijana wanakabiliana na vita ya hisia na mawazo mseto na kusababisha kuwapo msukumo mkali wa kujiingiza katika mapenzi au makundi yenye ushawishi usiofaa katika jamii.

"Ilikuwa ngumu sana wazazi kuielewa ndoto yangu ya kutaka kuwa mwanamziki ila walisisitiza sana kuheshimu shule na kujiepusha na makundi mabaya," amesema.

Mwanamuziki huyo yupo katika kampeni ya kipepeo inayoendeshwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ikishirikiana naTaasisi ya Benjamin Mkapa na kuratibiwa na Clouds Media



## Kwa hili, Mabeste pole yako

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Mabeste, ameibua mapya baada ya kudai kwamba mke wake kapata ujauzito na mwanamume mwingine ambaye alikuwa ni rafiki yake kipenzi.

Akizungumzia kuhusu taarifa hiyo, Mabeste ameeleza wakati wote alikuwa akijua ujauzito huo ni wake, lakini baada ya siku kupita alibaini kuna mwanamume mwingine mwenye uhalali na mtoto huyo.

"Kwenya maisha unapoishi unatakiwa utambue kwamba hii dunia kila mtu ana maono yake, kuna kitu unaweza ukaogopa kukifanya lakini kwangu inaweza ikawa nyepesi, kipindi kile tupo kwenye matatizo nilikuwa sijui kama anaujauzito ila nilikuwa nategemea, pia nilikuwa najua kama ujauzito sio wangu" amesema Mabeste





## Wolper unawazingua masharo wewe!

MWIGIZAJI wa Bongo Muvi, Jacqueline Wolper, ameibua jambo jipya baada ya kudai wanaume wa uswahilini ndio wanamvutia kimapenzi.

Hata hivyo, amewaponda vijana watanashati au masharobalo kwamba hawana lolote na kwamba hawajui nini maana ya maisha.

"Hakika huwa sipendagi wanaume mabishoo, napenda wanaume 'ma-gangster' au watoto wa kiswahili ndiyo mikato yangu, kwa sababu anajua nini maana ya maisha na sio bishoo, huwezi kunikuta nipo kwenye uhusiano na mtoto mzuri kwanza siwazimii naona wananipotezea muda" amesema Wolper.

# KIGOLI: Samaki mmoja akioza, wote wanatoa harufu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine unaweza kufanya kazi ambayo baadaye inaweza kuiangamiza familia yako, ndugu au jamaa yako. Kwa maana hiyo ni lazima kila mtu awe makini katika kutimiza wajibu wake, bila kuathiri upande mwingine.

Ukiiangalia filamu ya 'Kigoli' au kuisoma utakubaliana na hiki. Kuna makandokando mengi yamepita na kusababisha maafa makubwa.

Ni makosa ya mtu mmoja, lakini yamesababisaha mauaji ambayo yangeepukika.

Filamu imechezwa na Medebe Lidai, Hidaya Boli, Selemani Barafu, Riyama Ally, Leah Mussa na wengineo.

Hebu nikupe mchapo. Mzee Jitikavu amefiwa na kaka yake, ambaye amemuachia watoto wawili, Barafu, Sikudhani na shemeji yake.

Wote wanaishi kwake. Mzee Jitikavu baada ya arobaini akataka Barafu arithi mikoba ya uganga wa kaka yake, lakini Sikudhani ambaye alikuwa anasoma sekondari, aache shule awekwe ndani kama mwari, achezwe na kuolewa.

Awali walipata upinzani kutoka kwa mke wa kaka yake, yaani shemeji yake, pamoja na Sikudhani, lakini kwa sababu wote wanaishi kwake, hawakuwa na nguvu kubwa.

Upande wa pili kijana Korofindo ameishi na mkewe kwa miaka mingi bila kupata mtoto. Kutokana na hilo anaamua kuoa mke wa pili.

Dalali wa kutafuta mke wa Madebe. Anamsaka na kufika kwenye nyumba ya mzee Jitikavu ambako kuna mwari amewekwa ndani. Hii inakuwa faraja kwa Korofindo, na mzee Jitikavu. Kila kitu kinafanyika na sherehe za harusi zinafanyika kwa wengine furaha, wengine karaha.

Sherehe imekwisha, kila mtu kwake. Sikudhani akawa ameshajikatia tamaa ya kusoma, akaanza maisha mapya. Muda si muda 'kitumbo ndii' Miezi ya kujifungua ikapita. Mimba ikakaa hadi miezi kumi. Si hospitali dada, si kwa waganga, wapi. Ngoma ikawa ngumu.

Sikudhani nguvu zikamuishia akafariki dunia. Barafu alikuwa hamjui mke mkubwa wa Korofindo. Alipomuona na kujua kuwa ndiye mke wa shemeji yake, aliangua kilio. Hapa hapo kwenye msiba akawaambia watu kuwa yeye ndiye aliyemuua dada yake. Wote wakashtuka.

Kumbe Barafu baada ya kurithi mikoba ya baba yake, mmoja wa wateja walioenda kwake ni mke mkubwa wa Korofindo. Mke huyo alitaka mke mdogo afungwe na asizae kwa sababu anamkosha amani kwenya ndoa yake.

Bila kutambua kuwa mke huyo mdogo ni dada yake Sikudhani, akatengeneza dawa kuwa atazaa baada ya miezi 11 na siku ya tatu atakufa.





## Nuh bado amganda 'Shishi Baby'

MSANII wa BongoFleva, Nuh Mziwanda, amesema mchoro wa tattoo wenye jina la mpenzi wake wa zamani, Shilole, haumfanyi kujisikia vibaya.

Mziwanda, alichora tattoo ambayo ilisomeka "Shishi Baby" ambayo hadi leo bado unaonekana na kuwafanya mashabiki wake kuwa na maoni tofauti.

"Mimi nina tattoo nyingi sana, zote nazipenda huwa sichori kwa kuiga, kuhusu Shilole ni tattoo sio mwanamke, niliichora ukweli sikulazimishwa nilifanya hivyo kutoka ndani ya moyo wangu na nilikuwa najua kama kuna kuachana au kugombana," amesema Nuh Mziwanda.

# Ngoma tano kali alizoziacha Babu Njenje



**Na Adam Fungamwango**

ALFAJIRI ya Jumapili iliyopita, anga la muziki wa Tanzania liligubikwa na wingu zito kwa kuondokewa na mwanamuziki mkongwe Mabrouk Hamisi Omari maarufu kama 'Babu Njenje.'

Ni mwanamiziki aliyejizolea umaarufu mkubwa kwenye fani hiyo, hasa kwenye aina yake ya uimbaji wa nyimbo za mduara.

Babu Njenje aliyekuwa mwimbaji kiongozi wa bendi ya Kilimanjaro Revolution, alizikwa siku hiyo hiyo kwenye Makaburi ya Kisutu jijini Dar es Salaam na kuacha mke na watoto wawili.

Kwa mujibu wa mwanamuziki mwenzake, John Kitime ni kwamba, marehemu alikuwa akisumbuliwa kwa muda mrefu na ugonjwa wa kiharusi ambao ulisababisha ashindwe kuhudhuria maonyesho ya bendi hiyo.

Hizi ni baadhi ya nyimbo ambazo zilimfanya Babu Njenje kutamba na kupata umaarufu sana miaka ya '90 hadi mwanzoni mwa mwaka 2000.

### NJENJE

Huu wimbo ulitoka katikati ya miaka ya '90, na ndiyo ulioitambulisha bendi hiyo na kupata umaarufu mkubwa.

Mbali na hilo, umaarufu wa wimbo huu, ndiyo uliifanya bendi kuitwa jina la 'Wana Njenje', lakini pia muimbaji kiongozi marehemu, kupachikwa jina la 'Babu Njenje' pia.

"Njenje oo Njenje na kiparamoto Njenje. Kitamutamu cha boga, kutia nazi kunoga, mkono wataka kula, maungo yaona woga." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye kibao hicho, ulioimbwa na mtindo wa mduara.

### KINYAUNYAU

Kuonyesha kuwa hawakubahatisha, Babu Njenje na bendi yake ya Kilimanjaro walirudi na wimbo mwingine ambao nao ulitamba sana waliouita 'Kinyaunyau.' Nao pia upo kwenye mahadhi ya Mduara ambao ulizidi kumpa sifa.

"Kinyaunyau kikia cha pweza, mwataka mambo hamtayaweza." Ni sauti ya Babu Njenje ikihanikiza kwenye wimbo huo.

### KACHIRI

Mashabiki wa Babu Njenje na bendi hiyo walizidi kujipatia uhondo baada ya bendi hiyo kuibuka tena na kibao kingine kitamu kiitwacho 'Kachiri.'

Kama kawaida ni mtindo wa mduara ambao uliwachetua mashabiki wengi ambao wanajipanga foleni na kukaa mduara, huku mwenyewe akihanikiza mwishoni na kibwagizo kilichobeba zaidi wimbo huo.

"Kachiri Kachiri saga, mume wangu kasafiri, kaniachia kigoma na mtindo wa hariri, kaniachia korola na madola teletele, na kidani cha dhahabu na kiatu cha kokokoko, kisimu cha mkononi,

Buzi langu limo ndani nimelifunga kiguzoni, mchunaji una nini? katafute Vingunguti, buzi langu hulipati, Kachiri saga, Kachiri saga, Kachiri saga."

### NCHECHEME

Babu Njenje na Kilimanjaro Band walikuwa hawabahatishi. Yoyote aliyedhani walikwisha alikosea.

Baadaye wakatoka na ngoma nyingine waliyoiita 'Nchecheme' ambayo kama kawaida ilikuwa kwenye mahadhi ya mduara, iliyozidi kuwapa heshima na umaarufu

'Mama mwanangu leo, ukawacha napinda mgongo mie, kwani sina neno." maneno hayo yamo kwenye wimbo huo.

### NDEMBELE

Ni wimbo ambao pia uliimbwa na Babu Njenje, lakini huu ulikuwa tofauti kidogo kwani uliimbwa kwenye lugha ya Kisukuma mchanganyiko na Kinyamwezi, ingawa mipigo haikutofautiana sana na mduara.

# Majirani wamvuruga Burna Boy

MWANAMUZIKI wa Nigeria, amepatwa na mkasa mzito baada ya kukamatwa na polisi kufuatia majirani zake kulalamika anawapigia kilele.

Burna Boy, ametiwa nguvuni kutoka nyumbani kwake baada ya majirani hao kwenda polisi kulalamika kwamba hawapati usingizi kutokana na kelele zinazotoka ndani ya nyumba ya mwanamuziki huyo.

Baadhi ya video zilizosambaa katika mitandao ya kijamii, zinaonyesha majirani hao wakitoa malalamiko yao kutokana na kero za msanii huyo.





## EShun kwa nini uliyaweka moyoni?

MWANAMUZIKI na mshindi wa tuzo ya muziki ya Vodafone ya Ghana, eShun, amekiri kuwa na uhusiano wa kimapenzi na aliyekuwa meneja wake.

EShun amesema tukio hilo limefanyika miaka miwili iliyopita, lakini aliamua kukaa kimya kutokana na unyanyasaji uliofanywa na meneja wake huyo.

Amesema wakati huo alikuwa anafanyakazi katika lebo inayomilikiwa na mpenzi wake wa zamani, na ilikuwa vigumu kuepuka unyanyasaji wa kijinsia kutoka kwa meneja wake huyo.

## Mercy Eke kumbe wivu nawe unao

MSHINDI wa shindano la Big Brother Nigeria, Mercy Eke, amesema watu wafahamu kwamba huwa ana wivu sana katika mapenzi.

Mrembo huyo aliamua kuambia mashabiki wake katika ukurasa wake wa Twitter, kwamba mapenzi yanamfanya kuwa tofauti na wakati mwingine wivu wa kupindukia.

"Nina wivu katika mapenzi, hilo mliamini au hapana lakini nawapenda sana wote," amesema Mercy.





## Mjengo wa Khloe upo sokoni

MWANAMITINDO bilionea, Khloe Kardashian, ametangaza jumba lake la kifahari ameliweka sokoni baada ya kumiliki kwa miaka 20.

Nyumba hiyo maarufu kama Calabasas, aliinunua kutoka kwa mwanamuziki Justin Bieber kwa kiasi cha dola milioni 7.2 mwaka 2014, sasa inauzwa kwa bei ya juu ya dola milioni 19.

Kulingana na mtandao wa E!News, nyumba hiyo ambayo ipo katika eneo la heka mbili na inaelezewa kuwa ya gharama zaidi kuliko ilivyonunuliwa awali.

## Mercy Aigbe aonyesha jeuri ya fedha

MWENDO wa Mercedes Benz! Ndivyo mwigizaji wa Nigeria, Mercy Aigbe, alivyojipambanua kwamba siku hizi yupo juu kwani atakuwa akitembelea gari lake jipya aina ya Mercedes Benz Sports.

Mwigizaji huyo aliamua kuweka wazi katika mtandao wa Instagram, kwa kulionyesha gari hilo la kifahari lenye rangi nyekundu.

"Baada ya kazi ngumu, waheshimiwa tuungane na Benz Gang, ni usafiri wangu mpya," ameandika Mercy.



MAKALA



# Asilimia 25 ushuru kwenye chupa za kioo utavuruga biashara soko la Afrika Mashariki

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI karibuni Kenya ilifanya mabadiliko kwenye Sheria ya Biashara ya mwaka 2020 ikiwa ni mabadiliko ya Sheria ya Biashara ya mwaka 2015 na kuweka ushuru wa asilimia 25% kwa bidhaa za chupa za kioo zinazoingia nchini humo kuanzia Machi mwaka huu.

Chini ya sheria hiyo ya ushuru huo wa bidhaa hakuna msamaha wowote uliowekwa kwa bidhaa zinazouzwa nchini humo kutoka kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hivyo ushuru huo wa bidhaa kwa asilimia 25% utahusu pia bidhaa za chupa za kioo zinazoingizwa nchini Kenya kutoka Tanzania.

Ni dhahiri mabadiliko hayo yatasababisha ongezeko kwa gharama za bidhaa za chupa zinazoagizwa kutoka nje ya Kenya ikilinganisha na bidhaa za chupa za kioo zinazozalishwa na viwanda vya nchini Kenya.

Kampuni ya Kioo inauza bidhaa zake nchini Kenya hivyo ushuru huo wa asilimia 25% utasababisha bidhaa za chupa ya kioo kutoka Tanzania kushindwa kushindana kwenye soko la Kenya kwani bidhaa hiyo ya chupa inayotengenezwa Kenya itakuwa rahisi kuliko zile zinazoagizwa kutoka Tanzania.

Mwingiliano au utengamano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) unajumuisha kuanzishwa kwa Ushuru wa Pamoja na soko la Pamoja. Vifungu vya 75 na 76 vya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki vilihusisha kuanzishwa kwa ushuru wa pamoja na soko la pamoja.

Ushuru wa Pamoja ndiyo msingi mkuu wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) na ilianzishwa chini ya protokali ya Ushuru wa Pamoja.

Chini ya Itifaki ya Ushuru wa Pamoja nchi wanachama waJumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) zinapaswa kuimarisha biashara baina yao na miongoni mwa makubaliano ni kuondoa tozo za ndani na tozo mbalimbali na kupunguza vizuizi kwaajili ya kutengeneza mazingira bora ya biashara kwa ukanda huo.

Soko la pamoja lilianzishwa chini ya protokali ya kuanzishwa kwa Soko la Pamoja kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki lengo likiwa ni kurahisisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi wanachama kwa kutoa ushuru wa kuingizwa kwa bidhaa, fursa za kazi, huduma na mitaji kwa nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hatua ya Kenya kuweka asilimia 25% kwa bidhaa za chupa za kioo zinazotoka Tanzania inapingana na vifungu vya sheria ya mkataba na Itifaki ya Ushuru wa Pamoja.

Kenya ni soko muhimu sana kwa bidhaa za chupa za kioo zinazozalishwa Tanzania hivyo kwa kuweka kiwango hicho cha ushuru wa chupa za kioo zinazotoka kampuni ya Tanzania kama Kioo Limited, kutamaanisha kwamba bidhaa kutoka Tanzania zinakuwa ghali zaidi ya zile zinazozalishwa nchini Kenya.

> **Chini ya Itifaki ya Ushuru wa Pamoja nchi wanachama waJumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) zinapaswa kuimarisha biashara baina yao na miongoni mwa**

Hali hiyo itasababisha viwanda vinavyotumia bidhaa za chupa za kioo vya nchini Kenya kutoagiza tena chupa za kioo kutoka Tanzania kwani zitashindwa kushindana kwenye soko.

Hali hii itaathiri sana wanunuzi wa chupa za kioo kwani watalazimika kutegemea chupa za kioo zinazozalishwa nchini Kenya pekee ambako kuna wazalishaji wawili tu wa chupa za kioo ambao hata hivyo hawawezi kutosheleza mahitaji yote ya viwanda vya nchini Kenya.

Tanzania na Kenya zina usawa linapokuja suala la mfumo wa bei wa bidhaa na fursa za masoko. Wakati Tanzania kuna gesi asilia Kenya kuna magadi (Soda Ash) bidhaa ambazo zinaziweka nchi hizi kwenye nafasi nzuri ya kupunguza gharama za uzalishaji kwenye mataifa haya.

Kioo Limited inalipeleka suala hili kwenye mamlaka husika Tanzania na pia kwenye mahakama ya haki ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kuingilia haraka kwani wakati soko la bidhaa zake limeathiriwa kutokana na janga la Covid 19, ushuru huo wa bidhaa ni kama umetonesha kidonda.

Kioo Limited ni kampuni ya kizalendo ambayo imekuwa kwa muda mrefu ikizalisha bidhaa za chupa za kioo na kuuza ndani na nje ya Tanzania.

Kampuni hii imekuwa ikibadili malighafi zinazopatikana hapahapa nchini na kuzigeuza kuwa bidhaa zenye thamani kama ambavyo imekuwa ikisisitizwa na Rais wa awamu ya tano, Dk. John Pombe Magufuli katika hotuba zake mbalimbali kuhusu Tanzania ya viwanda.

Kioo ni moja ya kampuni kubwa ya kutengeneza chupa za kioo kwa ajili ya vinjwaji baridi kama soda, juice, bia, pombe kali na kwa ajili ya vyakula mbalimbali kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kati.

Mitambo ya Kioo Limited ni ya kisasa zaidi na yenye uwezo mkubwa sana katika ukanda mzima wa Afrika ambayo inauwezo wa kuzalisha bidhaa bora za chupa na kutoa fursa kwa wateja wake kupunguza gharama za uzalishaji mali kwa kutumia bidhaa zake, kwa muda wa miaka mitano iliyopita kampuni imeweza kuwekeza vya kutosha kwenye mitambo yake ili kuwa na uwezo wa kuzalisha bidhaa bora kwa wateja wake.

Kampuni hii imeajiri wafanyakazi zaidi ya 600 kwa ajira za moja kwa moja na zingine nyingi zisizo za moja kwa moja kwa wafanyakazi wanaosaidia shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kiwandani.

Kwa sasa mitambo yake inauwezo wa kuzalisha tani 400 za bidhaa za chupa za kioo kwa siku na inauza asilimia 60% ya bidhaa hizo nje ya nchi na kutosheza soko la ndani kwa asilimia 100% ya bidhaa za chupa kwa viwanda vya ndani ya nchi vinavyo tumia bidhaa hizi.

Kampuni ya kioo Limited ni miongoni mwa kampuni chache zinazouza nje bidhaa katika sekta ya uzalishaji hapa nchini, na imekuwa ikiingizia nchi fedha nyingi za kigeni.

MAKALA

## SIKU YA TUMBAKU DUNIANI

# Wanaharakati TTCF...
# Uzalishaji tumbaku mbadala kuziba pengo lake zao la kitaifa Ufuta, karanga, alizeti...

**Na Sabato Kasika**

TUMBAKU ni miongoni mwa mazao matano ya biashara ambayo serikali imeamua kuyawekea mkakati wa kuyaendelez, ili wakulima wanufaike na jasho lao, huku yenyewe ikikusanya kodi.

Mbali na tumbaku, mazao mengine makuu ya biashara kwenye mkakati huo ni pamba, korosho, chai na kahawa, yanatokusudiwa yawe na usimamizi katika uzalishaji.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa pamoja na kudhuru afya, kilimo cha tumbaku, uzalishaji wa bidhaa zake, namna zinavyotupwa, kwa ujumla zinaharibu matumizi mazingira.

Kutokana na athari hizo, bidhaa zake zimetengewa siku maalumu ya kimataifa inayoadhimishwa kupinga matumizi yake; Siku ya Kupinga Matumizi ya Tumbaku Duniani.

Hivyo, kesho Mei 31 tunaungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha siku hiyo, ikiwa na kaulimbiu ambayo tafsiri yake inayotamkwa kwa lugha ya Kiingereza 'protecting youth from industry manipulation and preventing them from tobacco and nicotine use.'

Ni dhana inayobeba tafsiri isiyo rasmi kwamba "kuwaepusha vijana kutumika katika viwanda vya kuzalisha bidhaa ya tumbaku na matumizi ya vimelea vya nikotini.'

Shirika la Afya Duniani (WHO), katika moja ya ripoti zake linasema zao la tumbaku linafahamika kwa kusababisha mmomonyoko wa ardhi na hata katika uzalishaji wa bidhaa zake.

Ufafanuzi wa WHO ni kwamba kuna taka nyingi wakati wa uzalishaji bidhaa zinazotumiwa na zinabakiza taka nyingi, takriban asilimia 40 ya taka zitokanazo na vishungi vya sigara zinaopatikana maeneo ya mijini.

Baadhi ya mikoa inayolima tumbaku, nayo imekuwa na uharibifu wa mazingira, unaotokana na ukataji miti kwa ajili ya kuni za kukaushia tumbaku.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba mara tumbaku inapovunwa, huwa inawekwa kwenye tanuru linalotumia kuni nyingi, ili kuwepo moto wa kutosha kwa ajili ya hatua mbalimbali za ukanushaji wa zao hilo.

Ili tumbaku ikauke, ni lazima miti yake ikatwe kwa wingi kupata kuni za kutosha, hali inayotafsiriwa ni uharibifu wa mazingira, ambao kimsingi unatakiwa kuachwa sasa.

Kutokana na uharibifu huo wa mazingira unaosababishwa na kilimo cha tumbaku, baadhi ya wadau wanaishauri serikali kutafuta zao mbadala la kimakakati linaloziba nafasi yake.



Mkulima wa tumbaku wilayani Mpanda.

WANAHARAKATI

Dk. Kokulinda Kagaruki, mwanakarakati wa kupinga matumizi ya tumbaku, anasema kuna mazao mengi yasiyo na madhara ya kiafya wala yasiyoharibu mazingira yanayoweza kuwa mbadala wa tumbaku.

Anataja baadhi ya mazao hayo kama karanga, ufuta, alizeti na mbaazi kuwa mojawapo linaweza kufanywa mbadala wa tumbaku.

Kagaruki, pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Kudhibiti Tumbaku Tanzania (TTCF), anataja mazao hayo yakipewa kipaumbele cha kitaifa yanaweza kuchangia uchumi wa taifa, pasipo kusababisha athari za mazingira na afya.

"Kwa mfano wataalamu wa afya wanasema, matibabu ya mgonjwa wa mishipa inayohusisha matumizi ya tumbaku, yanagharimu fedha nyingi hivyo ni muhimu kuepusha gharama hizo zisizo za lazima," anasema Dk. Kagaruki.

Ni kauli aliyotoa mwishoni mwa mwaka jana jijini Dar es Salaam, kwenye warsha ya waandishi kwa habari kuhusu ushawishi wa tumbaku na sera za afya nchini.

Katika warsha hiyo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) Prof. Mohamed Janabi, alitaja gharama ya kumtibu mtu ambaye mishipa yake imeharibika kwa sigara, ilikuwa ni Sh. milioni 30, ambayo ni kwa ajili ya kupata matibabu nchini India, hivyo kuna haja ya mbadala kudhibiti vyanzo tajwa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, mikoa inayojihusisha na uchumi wa kilimo cha tumbaku ni Tabora, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Kigoma, Katavi na Morogoro.

Anasema maeneo mengi katika mikoa hiyo, inafaa kulimwa mazao mbadala yanayostawi vizuri, pia soko zuri.

"Kwa kawaida tumbaku hustawi vema katika maeneo yenye mwinuko toka usawa wa bahari mita 900 hadi mita 1500, ingawa ipo myingine haistawi vizuri kwenye maeneo yenye mwinuko mita 1400 kutoka usawa wa bahari," anasema.

Anaeleza kwamba, karanga, ufuta na alizeti vinaweza kustawi kwenye maeneo hayo iwapo mojawapo litawekwa kwenye mkakati.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2018 zinaonyesha kuwa zaidi ya watu milioni 17.9 hufariki dunia kila mwaka kutokana na matumizi ya tumbaku.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alishatamka katika kila wagonjwa 100 wanaobainika kuwa na saratani, 32 saratani zao zimesababishwa na utumiaji tumbaku.

Katika hilo, Dk. Kagaruki anaitaka serikali iongeze juhudi zaidi katika kusimamia sheria na kutekeleza mkataba wa kimataifa unaowataka wavutaji tumbaku kutovuta maeneo yasiyoruhusiwa.



Uvutaji sigara ukiendelea. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**RAPHAEL JULIAS MTAMBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Carina SI yenye namba za usajili T828 ATX.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: CHA/RB/489/2019.

157563

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

AMOUR UTALI BAKAKI anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI yenye namba ya usajili na. T 438 BKV.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MAN/KIT/RB/395183/2020.

157564

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KERVIN ERNEST MOSHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 596 AWD TOYOTA CALDINA.** Chassis namba **ST21040331395.** Engine namba **357735118.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No. **9910812809976.**

157566

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 15 YA MWAKA 2020**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SELEMAN .M. KATIMBA …MAREHEMU**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**RASHID .S. KATIMBA ……….MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika Jalada za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 Mwezi wa Juni, 2020.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 21 Mwezi wa Mei, 2020.

NAIBU MSAJILI

157567

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA**
**YAH: SHAURI LA MADAI NAMBA 223 / 2020**

**MDAI……………ISIHAKA SHABAN**

**DHIDI YA**

**MDAIWA………………JAFARI SEFU**

Unaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Mjini Mwanza kufika tarehe 10/06/2020 saa 2:00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai yaliyofunguliwa hapa Mahakamani.

Endapo hutafika Mahakamani shauri litasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

*D.J.Butambala*
HAKIMU MKUU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
**MWANZA.**

HAKIMU MKUU
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANZA MJINI

157565

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 30-05-2020

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 30-05-2020 kampuni ya ESTIM CONSTRUCTION CO. LTD itasafirisha Mzigo Excarator Machine wenye vipimo vikubwa kutoka Mwenge kuelekea Dar es salaam Port kupitia Sam Nujoma, Nelson Mandela na barabara ya Kilwa. Gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 530 ATG / T 911 ADC**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - mita | 22.00 |
| Upana | -mita | 3.1 |
| Kimo | -mita | 4.8 |

3. Njia itakayotumika: Mwenge hadi Dar es salaam Port kupitia Sam Nujoma, Mandela na barabara ya Kilwa.

   Magari yatasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

157568


**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# KLABU ZAMPA PRESHA SANCHO




**DORTMUND,** Ujerumani

JADON Sancho anahisi presha kubwa kutokana na kuhusishwa na klabu kubwa kubwa nyingi, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa Borussia Dortmund, Thomas Delaney.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England, Sancho, amekuwa akivumishwa kutakiwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England pamoja na wapinzani wa nyumbani wa Dortmund, Bayern Munich baada ya kuwa na msimu mwingine wa kuvutia kwenye Bundesliga.

Amefunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho jumla ya 30 kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani msimu huu, akiwa nafasi ya pili nyuma ya nyota wa RB Leipzig, Timo Werner.

Delaney anaamini kwamba Sancho atakuwa mmoja wa wachezaji watano wa juu duniani, lakini amebainisha kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 tayari anahisi kuwa na presha kwa kuhusishwa kwake na klabu kubwa.

"Yeye ni mmoja wa wachezaji wenye vipaji vikubwa niliowahi kucheza nao," amesema akiiambia ESPN's Gab & Juls podcast.

"Kwa kipaji alichonacho presha nyingi inakuja kwake, na nafikiri taratibu anaanza kuhisi hivyo kwa timu ya taifa ya England na klabu zinazomzunguka."

# Ningejaribu kumsajili tena Neymar – Rais Barca

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa zamani wa Barcelona, Sandro Rosell amesema angejaribu kumsajili nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar kama mchezaji wake bora zaidi wa pili duniani nyuma ya Lionel Messi.

Neymar aliondoka Barca kwenda PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya duniani ya euro milioni 222 mwaka 2017, lakini fowadi huyo ameendelea kuhusishwa na kurudi pale Camp Nou.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alishindwa kurudi kwa mabingwa hao wa LaLiga, Barca mwanzoni mwa msimu wa 2019-20 na ameripotiwa kuwaniwa tena.

Rosell mwenye umri wa miaka 56 alikuwa Rais wakati Barca walipomsajili Neymar kutoka Santos mwaka 2013 na sasa ameahidi kumrudisha tena mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil.

"Kama ningekuwa rais wa Barca, ningejaribu kumsajili Neymar," amesema Rosell akiiambia COPE na redio Marca.

"Yeye ni mchezaji wa pili bora zaidi duniani baada ya Messi na anafiti vizuri sana kwenye falsafa ya klabu."

Tangu alipoondoka PSG, Neymar ameshinda mataji matatu mfululizo ya Ligue 1, Kombe la Ufaransa na Kombe na Ligi.







# *Harry Kane ashauriwa kubakia Spurs*

**LONDON,** England

HARRY Kane hahitaji kuondoka Tottenham kushinda mataji, kwa mujibu wa mshambuliaji wa zamani wa klabu hiyo, Jurgen Klinsmann.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England bado hajashinda taji lolote kubwa na Tottenham na alibainisha Machi, mwaka huu kwamba anaweza kufikiria kuondoka kama anahisi klabu haijiimarishi kushinda kitu.

Dimitar Berbatov na Teddy Sheringham wote wameshauri Kane kufikiria kuondoka Spurs kwenda Manchester United, kama wao walivyofanya wakati wakicheza hapo, kama anataka kunyanyua mataji.

Klinsmann pia aliondoka pale London Kaskazini wakati akiwa kwenye kiwango cha juu na kujiunga na Bayern Munich, lakini anashawishika Kane anaweza kupata mafanikio na kutimiza malengo yake chini ya Jose Mourinho.

"Anaweza kufanikiwa kitu fulani," amesema Klinsmann akiiambia talkSPORT.

"Anakipaji, na sasa yupo katika kilele cha juu kabisa katika uchezaji na naamini anaweza kushinda kitu fulani pale."

HABARI MICHEZO

# Nywele za Firmino zamshangaza Robertson

**LIVERPOOL,** England

MUONEKANO mpya wa staili ya nywele za Robert Firmino umeonekana kumshangaza mchezaji mwenzake wa Liverpool, Andy Robertson.

Baada ya miezi miwili ya kutotoka ndani kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, wachezaji wa Liverpool walirudi kwenye mazoezi pale Melwood wiki iliyopita wakijifua kwa makundi madogo.

Muonekano wa wachezaji wengi wa wekundu hao umekuwa wa aina yake, huku wengi wakiwa wameachia nywele kwa staili, baada ya saloon nyingi kufungwa nchini England kutoka na watu kutotakiwa kutoka nje.

Adam Lallana, Sadio Mane na Alisson Becker wote wamekuja na muonekano mpya wa nywele, lakini rasta ndefu za Firmino zimemshangaza zaidi Robertson.

"Kuna maswali mengi," alinukuliwa Robertson na tovuti ya klabu. "Alisson nywele zake zimeonekana kuendelea kukua na kukua – sijui kama atakuwa hivyo hadi tukapoanza kucheza!

"Lakini za Firmino zimeniacha hoi. Mara zote yeye ananyoa, lakini sasa ameziachia na kumfanya awe na muonekano wa ajabu."



# HAALAND KUTUA EPL NI SUALA LA MUDA




**DORTMUND,** Ujerumani

ERLING Haaland mwishowe atakwenda kwenye Ligi Kuu England, lakini straika huyo wa Borussia Dortmund hawezi kuharakisha uhamisho wa kwenda England, kwa mujibu wa Jan Aage Fjortoft.

Fjortoft, ambaye alicheza mechi 71 kwa timu ya taifa ya Norway pamoja na klabu za Ligi Kuu England, Middlesbrough na Barnsley, amekuwa akivutiwa zaidi na raia mwenzake huyo.

Haaland na timu yake ya utawala wamechagua kuwa makini katika soka la uhamisho, licha ya klabu kadhaa za England kumhitaji.

Manchester United walikuwa wa kwanza kuwania saini ya nyota huyo wa Norway kabla ya uhamisho wa kwenda Dortmund kutoka Salzburg kwa euro milioni 20 katika uhamisho wa Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 amefunga mabao 13 katika mechi 14 katika mashindano yote kwa Dortmund na Fjortoft anafikiri kuchomoza kwa kasi zaidi msimu huu kumemshangaza.

"Tunafurahia na kile kinachofanywa na Erling na timu yake imechagua sehemu ambayo ataimarika zaidi kama mchezaji," amesema Fjortoft akiiambia Sky Sports.

"Alikwenda kutoka Molde – ambako Ole Gunnar Solskjaer alikuwa kocha wake, hivyo unaweza kufikiria namna gani ugumu uliokuwapo kwa yeye kutokwenda Manchester United na kuamua kwenda Dortmund."

# *Balotelli rasmi kuondoka Brescia*

**BRESCIA,** Italia

RAIS wa Brescia, Massimo Cellino anatarajia Mario Balotelli ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu.

Balotelli alisaini mkataba wa miaka mitatu kucheza katika klabu hiyo ya mji wa nyumbani kwake mwaka jana, lakini hakuwa kwenye kiwango kizuri kwenye Serie A na mlolongo wa matukio ya utata nje ya uwanja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia alibwatukiana na kocha wake mkuu wa zamani, Fabio Grosso Novemba, mwaka jana na alimwambia ataondoka Januari baada ya kushindwa kuelewana na rais wa klabu, Cellino.


Alibakia kwenye uwanja huo wa Mario Rigamonti lakini alishindwa kufunga katika mechi sita kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona na ameripotiwa kutoonekana kwenye mazoezi Jumanne.

Cellino anatarajia wataachana na Balotelli mwishoni mwa msimu huu.

"Hana tena mpango na sisi na naona ni bora tu aondoke kwani tumeshafikia makubaliano hayo."

Balotelli amefunga mabao matano katika mechi 19 alizoichezea Brescia msimu huu na Cellino anatambua kwamba mchezaji huyo hajawatimizia kile walichokipanga.

"Nampenda na niliamini angeweza kufanya kitu fulani hapa klabuni kwetu, lakini amenikatisha tamaa sana."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BALE AENDELEA KUIVURUGA REAL

**●●● Ni kutokana vigogo hao kutopokea ofa yoyote kuhusiana na winga huyo...**

**MADRID,** Hispania

SINTOFAHAMU ya Gareth Bale ndani ya kikosi cha Real Madrid inatarajiwa kuendelea tena katika majira ya joto baada ya klabu hiyo kutopokea ofa yoyote kuhusiana na mchezaji huyo wakati dirisha la usajili likikaribia kufunguliwa, taarifa mbalimbali zinaeleza.

**Winga huyo wa Timu ya Taifa ya Wales aliwahi kuhusishwa na kutakiwa na Manchester United na Tottenham, lakini atalazimika kubakia kwa vigogo hao wa LaLiga katika kipindi cha miaka miwili kilichobakia kwenye mkataba wake.**

Gazeti la Marca linaamini hakuna klabu iliyowasilisha ofa ya kumhitaji winga huyo mwenye umri wa miaka 30 kuondoka katika klabu hiyo ya Hispania.

Liliendelea kuandika kuwa hakuna uhakika kama winga huyo atatakiwa na klabu nyingine kwa sababu inaonekana hayuko tayari kujiunga na timu nyingine kwa wakati huu.

Sakata hilo la Bale linaonekana litaendelea kudumu mpaka muda wa mkataba wake utakapomalizika hapo Bernabeu na hatimaye kuondoka kama mchezaji huru.

Hata hivyo uamuzi wa kuendelea kubakia hapo hauungwi mkono na mashabiki wa Real ambao hana husiano nao mzuri, lakini analazimika kubakia kutokana na kubanwa na vipengele vya mkataba.

Licha ya winga huyo wa zamani wa Southampton ambaye analipwa mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki kufunga bao katika mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kubeba kikosi, bado hana thamani kwenye klabu hiyo.

Kwa sasa Bale amekiri kuwa amepoteza hali ya kujiamini kila anapoingia uwanjani Bernabeu kwa sababu ya kuzomewa na mashabiki wa timu hiyo. Akizungumza katika kipindi cha Erik Anders Lang alisema: "Tunakuwa kwenye presha kubwa katika kila mechi. Kama huchezi vizuri, unakumbana na hali ya kuzomewa.

"Ninakumbana na watu 80,000 uwanjani ambao wananizomea kwa sababu sichezi vizuri. Nimekutana na hili kwa muda mchache, si vizuri na haiwezi kuimarisha uwezo wako wa kujiamiani kwa siku zijazo.

Hatima yake ndani ya Real haionekani kama ni mchezaji anayepewa nafasi na licha ya mechi za LaLiga zinatarajiwa kurejea, na Zinedine Zidane hana uhakika kwa kumtumia na anahesabika kama mchezaji wa akiba kwenye hatua hii ya lala salama.

Hali ya kuandamwa na majeruhi ilimfanya Bale asiwe kwenye mipango ya ushindi ya kocha huyo, akiwa ametumia kwenye michezo 18 katika mashindano yote msimu huu.

## ZISIKUPITE

### LEICESTER YAMTAKA LALLANA

LEICESTER imewasilisha ofa ya mkataba mrefu kwa Liverpool ili kumsajili kiungo wake, Adam Lallana. Nyota huyo wa kikosi cha Timu ya Tifa ya England mwenye umri wa miaka 32 anatarajia kumaliza mkataba wake na klabu hiyo ya Anfield Juni, mwaka huu. ***(Football Insider)***

### COUTINHO AGOMBEWA EPL

KLABU tano za Ligi Kuu England ambazo ni Chelsea, Newcastle, Manchester United, Arsenal na Leicester wameonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Barcelona, Philippe Coutinho (27). Thamani ya Mbrazil huyo ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Bayern Munich ni pauni milioni 90. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### UNITED, NEWCASTLE VITANI

MANCHESTER United na Newcastle zimeonyesha nia ya kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Facundo Pellistri. Chipukizi huyo mwenye umri wa miaka 18 sasa anaichezea Penarol. ***(Mail)***

### FRASER AGOMBEWA ULAYA

MABOSI wa Galatasaray wameweka wazi nia ya kumsajili winga wa Bournemouth, Ryan Fraser. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 na raia wa Scotland anatajwa kuwindwa na Arsenal na Tottenham. ***(Daily Record)***

### IGHALO MAMBO SAFI

SHANGHAI Shenhua imeonyesha nia ya kukubali kumruhusu straika wake Mnigeria Odion Ighalo kuongeza mkataba mpya wa kuitumikia Manchester United. ***(ESPN)***

### PSG, ICARDI SAFI

PARIS St-Germain inakaribia kukamilisha mchakato wa kumpa mkataba wa kudumu straika wake, Mario Icardi. Nyota huyo raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 27, yuko kwa mkopo PSG akitokea Inter Milan lakini mkataba huo unamalizika kesho. ***(Sky Sports)***

### WILLIAN ANUKIA PSG

PSG inajiandaa kumsajili kiungo mchezeshaji wa Chelsea, Willian. Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 31 anatarajiwa kuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Le10Sport - in French)***

### LIVERPOOL HATARINI

HUENDA Liverpool ikacheza mechi zake zilizobakia kwenye uwanja huru, wakati tayari imeelezwa Ligi Kuu England itarejea tena kuanzia Juni 17, mwaka huu. ***(Times - subscription required)***

### YOUNG KUULA INTER

INTER Milan inatarajia kumwongezea mkataba beki wa zamani wa Manchester United, Ashley Young. Nyota huyo raia wa England ambaye ana umri wa miaka 34, alijiunga na klabu hiyo ya Italia Januari kwa mkataba mfupi wa miezi sita. ***(Telegraph - subscription required)***

### SANCHO APATA HOFU

INAELEZWA kuwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho anasikia hali ya wasiwasi kutokana na kuhusishwa kutakiwa na klabu nyingine mbali na Borussia Dortmund, mchezaji mwenzake, Thomas Delaney, amesema. Sancho (19), anawindwa zaidi na Manchester United. ***(ESPN)***

HABARI MICHEZO

## Polisi Tanzania yaikumbuka ligi

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema kikosi chake kimeimarika na kiko tayari kushuka dimbani kumalizia mechi za Ligi Kuu Bara zilizobakia.

Malale (pichani) aliliambia gazeti hili wachezaji wake 26 wameshaingia kambini na wanaendelea na mazoezi kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu katika kila mechi watakayocheza.

Malale alisema kikosi chake kina wakosa nyota watatu tu, lakini uongozi wa timu hiyo una taarifa za wachezaji hao ambao hawajaripoti kambini.



" Kabla ya kuanza mazoezi tulilazimika kuwapima afya zao wachezaji wote, ikiwamo uzito pamoja na joto, tunashukuru tumekuta wako sawa. Pia tumweweka utaratibu wa kunawa mikono kabla na baada ya kumaliza mazoezi kwa kutumia vitakasa mikono ili kujikinga na corona," alisema Malale.

Aliongeza kwa sasa timu yake inasubiri ratiba kutoka Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na wanaamini shirikisho hilo litatoa ratiba rafiki kwa klabu zote kwa kuzingatia muda uliobakia.

Naye Msemaji wa timu hiyo, Frank Lukwaro alisema wachezaji ambao hawajaripoti mpaka sasa wana matatizo ya kifamilia.

"Wachezaji ambao hawajaungana na wenzao wametoa taarifa, wana sababu za msingi za kuchelewa, tumewapa ruhusa maalumu lakini tunawatarajia hivi karibuni," alisema Lukwaro.

## Coastal Union yaitazama Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuwa na matokeo mazuri msimu huu ukilinganisha na miaka ya nyuma, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema malengo yake ni kumaliza Ligi Kuu Bara wakiwa ndani ya nafasi tano za juu.

Coastal Union ambayo imecheza mechi 28, ina pointi 46 na katika msimamo wa ligi iko kwenye nafasi ya nne nyuma ya vinara Simba wenye 71, Azam FC ( pointi 54), Yanga (pointi 51) na Namungo FC yenye pointi 50.

Mgunda alisema kikosi chake kimeshaanza mazoezi ya pamoja na amefurahishwa na kasi ambayo amewakuta nayo wachezaji wake.

Kocha huyo alisema mechi zilizobakia katika Ligi Kuu Bara ni chache lakini lolote linaweza kutokea kwa watakaofanya vizuri na watakaoharibu.

"Tumejipanga, lengo ni kumaliza msimu tukiwa katika nafasi tano za juu, tunaamini hili linawezekana kama hatutabweteka, ligi ni ngumu na huku tunakoelekea ndio pagumu zaidi," Mgunda alisema.

Aliwataka wachezaji wake kuendeleza 'moto' waliouwasha katika mzunguko wa kwanza ili kujiweka kwenye nafasi salama.

# SIMBA YAFURAHI SERIKALI KURUHUSU WASHANGILIAJI

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wamefurahishwa na uamuzi uliofanywa na serikali wa kuruhusu mashabiki kuingia viwanjani kushangilia wakati wa mechi za ligi hiyo zinazotarajiwa kufanyika kuanzia Juni 13, mwaka huu.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema timu zingekuwa na wakati mgumu endapo zingecheza mechi bila ya mashabiki.**

Manara alisema Simba imefurahia uamuzi huo na inawataka wanachama na mashabiki wote wa soka nchini kuhakikisha wanafika uwanjani kwa kufuata tahadhari zilizotolewa na wataalamu wa afya.

"Serikali yetu ni sikivu, inashaurika na inakubali ile dhana ya kukosoana, baadhi ya watu mitandaoni walinilaumu kwa ushauri wangu huu, lakini leo taarifa iliyosainiwa na mawaziri wenye dhamana ya michezo na afya nchini wamesaini tamko lenye kuafiki uwapo wa mashabiki viwanjani, ila sasa watalazimika kukaa umbali wa mita moja moja," alisema Manara.

Alisema wanafurahi kuona serikali imeelekeza namna mashabiki, wachezaji na viongozi wa soka na michezo mingine wanavyopaswa kuchukua tahadhari kuhusiana na ugonjwa wa corona.

"Hii ndio serikali sikivu tunayoizungumzia, inayokubali kushauriwa na watu wa kawaida," Manara alisema.

Pia kiongozi huyo alimpongeza Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe kwa kukubali kuondoa ukomo wa mashabiki kama ilivyokuwa awali na pia Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu kwa kuliongoza vema taifa katika mapambano hatari dhidi ya Covid 19.

"Sasa ni wajibu wetu mashabiki tutakaokwenda viwanjani kuzingatia masharti hayo ya kitaalamu ili nchi yetu iendelee kuwa salama zaidi," alisema Manara.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), linatarajia kutangaza ratiba mpya ya mechi zilizosalia za Ligi Kuu ambayo inashirikisha klabu 20 kutoka mikoa mbalimbali.



Wachezaji wa Simba wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Bara ambazo zinatarajiwa kuendelea kuanzia Juni 13, mwaka huu. **PICHA: SIMBA SC**

# *Nahimana ajiweka njia panda KMC*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa KMC FC ya jijini Dar es Salaam, umesema hatima ya kipa wao Mrundi Jonathan Nahimana ipo mikononi mwa Kocha wao Mkuu, Haruna Harerimana, imefahamika.

KMC haikufurahishwa na uamuzi wa Nahimana kutamka kwenye vyombo vya habari anapenda kujiunga na Simba, hali ya kuwa bado ana mkataba na klabu hiyo ya Manispaa ya Kinondoni.

Mwenyekiti wa Bodi ya KMC, Benjamin Sitta, alisema Nahimana ni kipa mzuri lakini uamuzi wa kuendelea kuitumikia timu hiyo katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania utaamuliwa na benchi la ufundi.

Sitta alisema uongozi umekuwa ukifanya kazi kwa ukaribu na kufuata mapendekezo kutoka kwenye benchi la ufundi kwa sababu ya kufikia malengo.

"Suala la kauli yake ya kutamani kuichezea Simba aliyoitoa hivi karibuni kipa huyo, tayari ameandikiwa barua ambayo nayo amejibu kwa kuomba msamaha, hivyo suala hilo lipo katika uongozi na kufanyiwa kazi."

"Na kuhusu mkataba wake ni kweli unamalizika mwisho wa msimu huu (Juni 30, mwaka huu), hatima ya kubaki au kuondoka itakuwa chini ya mwalimu, akimhitaji hatutakuwa na pingamizi," alisema Sitta.

KMC yenye pointi 33 baada ya kucheza mechi 29, ipo katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoongozwa na mabingwa watetezi, Simba huku Singida United ya Singida ikiburuza mkia.

# Michezo

Jumamosi Mei 30, 2020

Nipashe




Bale aendelea kuivuruga Real

UKURASA 22



Wachezaji wa Yanga wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu kwenye Uwanja wa Chuo cha Sheria, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA : JUMANNE JUMA**

## Sven: Hatima ya Ajibu Jumatatu

**Na Mwandishi Wetu**

MBIVU na mbichi kuhusiana na kiungo wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Ibrahim Ajib, itajulikana keshokutwa, imeelezwa.

Ajibu aliondolewa katika kambi ya vinara hao wa Ligi Kuu Bara baada ya kuchelewa kufika kwenye mazoezi yaliyoanza Jumatano.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, alisema baada ya mchezaji huyo kuchelewa, aliondolewa kwenye kikosi kutokana na kosa la uchelewaji.

"Ajibu si sehemu ya kikosi chetu kwa sababu alichelewa kufika katika siku ya kwanza ya mazoezi Jumatano, atarejea Jumatatu kama mambo yatakwenda vizuri," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa kikosi chake kinaendelea vema na mazoezi na amekuwa na programu za aina tatu tofauti, lakini amefurahi kufahamu tarehe rasmi ya kurejea kwa ligi hiyo.

Aliwataja wachezaji watatu ambao bado hawajaripoti ni Francis Kahata, Clatous Chama na Sharaf Shiboub, ambaye kwao Sudan bado wako kwenye 'lockdown' kubwa.

# Simba, Azam patachimbika

**Na Somoe Ng'itu**

### ●●● Ni katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la FA, 'dabi' nyingine yanukia karibuni...

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba watakutana na Azam FC katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA wakati watani zao, Yanga watawakaribisha Kagera Sugar.

**Mechi hizo za hatua ya robo fainali ya mashindano hayo ambayo hutoa tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, zimepangwa kufanyika kati ya Juni 27 na 28, mwaka huu jijini Dar es Salaam.**

Awali kabla ya kutokea kwa janga la ugonjwa wa corona (COVID 19), fainali za michuano hiyo ambayo bingwa mtetezi ni Azam FC, ilipangwa kufanyika Mei 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, mkoani Rukwa.

Kwa mujibu wa ratiba ya mashindano hayo iliyopangwa jana, endapo vigogo hao wa soka nchini watasonga mbele, basi watakutana kwenye hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo.

Akizungumza baada ya ratiba hiyo kutoka, Mwakilishi wa Simba, Khamis Kisiwa, alisema nia ya timu yake ni kupambana na hatimaye kuchukua kikombe cha mashindano hayo.

"Nia na madhumuni ni kuchukua kikombe, sio hiki, hata hicho ambacho wanafikiri tutalegezalegeza, nia yetu ni kuchukua vikombe vyote viwili," alisisitiza Kisiwa.

Aliongeza katika mchezo uliopita, walipanga kupata ushindi kwa penalti lakini sasa wataingia tofauti zaidi.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani wa pande zote mbili na hatuna timu ndogo kati ya hizo mbili.

"Ni robo fainali nzuri, inakutanisha mkubwa na mkubwa mwenzie, kwa sababu wote sisi ni wakubwa, mechi zetu zote na Simba zimekuwa na ushindani, itakuwa mechi nzuri, lakini kila mmoja atapambana ili aweze kwenda kuchukua kikombe hiki," Popat alisema.

Popat alisema nguvu zao zote wamezielekeza kwenye mashindano ya Kombe la FA baada ya kuona nafasi yao ni finyu kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

Mechi nyingine za hatua ya robo fainali ya michuano hiyo itakuwa ni kati ya Namungo FC ya Lindi dhidi ya Alliance FC kutoka jijini Mwanza wakati Sahare All Stars ya Tanga itapambana na Ndanda FC ya Mtwara.

Meneja Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto, alisema jana timu zote nane zinatakiwa kujiandaa vema kuelekea michezo hiyo kwa sababu hatua waliyofika ina ushindani zaidi.

Kizuguto alisema shindano hili limeendelea kuwa na ubora wa hali ya juu na timu mbalimbali zimefanikiwa kushinda kombe la mashindano haya.

"Timu tunaziomba zijiandae, ziwe tayari na mashindano haya, yoyote atakayekuwa amejiandaa atafanya vizuri, kama TFF tumejiandaa kucheza kwa kufuata mwongozo ambao tunausubiri, hatua hii si nyepesi, hatua hii si ndogo, mshindi wa mashindano haya ataiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa," alisema Kizuguto.

Aliongeza mechi za mashindano hayo zitakuwa nyumbani na ugenini, lakini hii itatangazwa baada ya kupata mwongozo rasmi kutoka kwa idara husika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >